ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu – Tarehe 17 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe pamoja na ratiba inaonesha kwamba ni Afisi ya Katiba na Sheria lakini kwanza itafuata Afisi ya Rais Tawala za Mikoa kwa dharura maalum. Mhe. Waziri tafadhali.

Ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri swali hili limeulizwa na Mhe. Mjumbe ambaye anahusika na yupo. Kwa hivyo, bahati mbaya hujamwita Mhe. Abdalla Maulid Diwani kutokana na mabadiliko.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe sasa swali namba 45 litaulizwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Nam. 45

Kutozingatia Usafi katika Mji wa Zanzibar

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Mji wa Zanzibar ni miongoni mwa miji ya kihistoria duniani ikiwemo Urithi wa Mji Mkongwe, lakini bado suala la usafi katika mji huu halijadhibitiwa ipasavyo vikiwemo vitendo vya watu kujisaidia haja ndogo pahala popote.

Je, hakuna sheria inayokataza jambo hilo la kujisaidia ovyo ambalo ni aibu kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 kama ifuatavyo lakini kwanza naomba kutoa maelezo mafupi:-

Mhe. Mwenyekiti**,** nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba, Mji wa Zanzibar ni miongoni mwa Miji Mikongwe duniani iliyoorodheshwa kuwa ni Urithi wa Dunia. Hii ni heshima kubwa ambayo Wazanzibari sote tunapaswa kuitambua, kuithamini na kuienzi hasa katika suala zima la kutunza usafi na mazingira ya mji.

Naomba pia nikiri kwamba pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali kupitia Baraza la Manispaa ya Mijini za kuuweka mji wetu katika hali ya usafi, kwa bahati mbaya sana bado kuna baadhi ya wananchi wanaendelea kuwa kikwazo katika kufikia lengo la kuupendezesha mji wetu. Hili linafanyika kwa namna tofauti ikiwemo suala la kujisaidia ovyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 45 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** Sheria na Kanuni zenye kukataza vitendo vya watu kujisaidia haja ndogo mahala popote zipo na zimekuwa zinatumiwa na Baraza la Manispaa ya Mjini katika kukabiliana na tabia hiyo mbaya. Aidha, zipo Sheria ndogo (*by-law)* ya mwaka 2004 ya udhibiti wa maeneo ya wazi na Sheria ndogo ya mwaka 2006 inayohusu makaro, michirizi, vyoo na taka. Sheria hizi zote zipo ili kudhibiti vitendo vya uchafuzi wa mazingira likiwemo suala la kujisaidia ovyo ambalo ni aibu mbele ya macho ya watu waliostaarabika.

Mhe. Mwenyekiti**,** Baraza la Manispaa ya Mjini pia limekuwa likitumia Sheria za Mamlaka nyengine pale inapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo kwa kuzingatia ukubwa wa kosa lenyewe. Kwa mfano, Sheria ya Afya ya Jamii na Mazingira Nam. 11 ya mwaka 2012 (*Public and Environmental Health No. 11 of 2012)* ni moja wapo ya Sheria zinazotumiwa na Baraza la Manispaa kukabiliana na tabia hiyo.

Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya serikali niipongeze sana na kwamba serikali iko makini ina sheria kali.

(a) Je, kama sheria hizi zipo na kanuni zipo ni watu wangapi ambapo wametiwa nguvuni kwa sheria hii.

(b) Kama tunakumbuka kwamba katika miezi michache iliyopita kuna taasisi ilijitolea kufanya usafi katika Mji Mkongwe kwa kuwa ni kioo cha Zanzibar kwa wageni wanaoingia nchini. Je, serikali au wizara yako ililichukulia vipi suala lile kurudia tena kufanya usafi ili iwe endelevu katika kusafisha Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni watu wangapi ambao wamefikishwa katika vyombo vya sheria. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba katika kukubaliana na kadhia hiyo zipo kesi ambazo tayari washukiwa wameshafikishwa katika vyombo sheria katika kipindi cha kutoka Januari 2017, kuna watu 14 ambapo kuna kesi ambazo zimepelekwa katika Mahakama ya Mwanzo Malindi baada ya watu hao kukamatwa na makosa ya kujisaidia ovyo katika maeneo ya mjini.

(b) Kuhusu taasisi ambayo ilikuwa inafanya usafi katika maeneo ya mjini na baadae kuondoshwa na sasa hivi kutaka kurejeshwa. Niseme Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mwakilishi kuhusu suala la taasisi ambazo zinafanyakazi tunaenda kwa muongozo na taratibu na kanuni zilizopo au sheria zinazotumika katika Mabaraza yetu.

Hivyo nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba taarifa hii bado sijaipata ipasavyo na kwa mantiki hiyo nitaifuatilia ili kuona kwamba tunampa majibu ambayo yako sahihi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mwanana kabisa ambayo ameyatoa katika swali hili namba 45.

Naomba nitoe majibu ya ziada ya swali la Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Jang'ombe.

(a) Ni kweli kabisa zipo kanuni, zipo sheria kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri na kama alivyosema katika kuwachukulia hatua watu hao 14, wamechukuliwa hatua na kufikishwa kwenye Mahakama na watu hao waliweza kupatikana na hatia na wakatozwa faini ya shilingi elfu hamsini kila mmoja.

(b) Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri ni kwamba taasisi inayojitegemea au iliyojitolea kwa hiari ni Taasisi ya G1. Kwanza nataka nimpongeze Mhe. Abdalla Maulid Diwani ambaye ni kiongozi wa taasisi hiyo kwa umahiri na umakini wake wa kuona kwamba suala la usafi wa mji linawahusu wananchi wote.

Kwa hivyo, nimpongeze na pale atakapokuwa tayari kwa mara nyengine tena Baraza la Manispaa au Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote nchini ziko tayari kushirikiana na taasisi kama hizo za kujitolea kwa ajili ya kuimarisha usafi ndani ya miji yetu.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, maradhi ya mripuko yanatokana na mkusanyiko au na mambo ya kujisaidia ovyo katika maeneo yetu na kwa bahati mbaya tuna vituo vingi vya daladala Michenzani, Mwembeladu, Mikunguni, Darajani na kwengineko, vituo hivi hakuna huduma hiyo ya kupata vyoo, pindi mtu akikutwa na dharura ya kutaka kujisaidia.

Je, kwa kuwa hili ni kero na aibu katika nchi yetu, Wizara ina mpango gani wa kulifanyia japo eneo kidogo tu likapatikana huduma hiyo pindi mtu anapokutwa na kadhia ya kutokea na haja kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika suala la miripuko ni jambo ambalo linaweza likatokezea kama itakuwa hakuna juhudi ambazo zinakuwa zikichukuliwa kwa upana wake.

Lakini pamoja na maelezo hayo ni kwamba juhudi kupitia Baraza la Mji zimekuwa zikichukuliwa katika kuona kwamba maeneo ambayo ni stahiki katika kuweka au kuona kwamba kunahitajika mahitaji haya ya kujenga vyoo, basi ziweze kufanyika ili kuona dhamira ya serikali kuona kwamba inaweza kukinga wananchi wake na majanga mbali mbali yanayotegemewa au na yale hayawezi kutegemewa basi ni kubwa, na kwa mfano katika Baraza la Manispaa

la Mjini katika juhudi zake za kuimarisha mazingira na miundo mbinu ya huduma ya vyoo hapa mjini vyoo 11 vimeweza kujengwa katika maeneo na mitaa mbali mbali kwa ajili ya jamii kupata huduma ya kujisaidia.

Kwa mfano katika maeneo ya Darajani, Marikiti Kuu, Forodhani, Shangani, Malindi na Mnazi Mmoja, Bustani ya *Jamhuri Garden* na Kinazini, vyoo 11 tayari vimeshajengwa na hatua mbali mbali na mahitaji katika maeneo mengine ambayo yanaonekana kunahitajika huduma hiyo, basi serikali haitosita kuona kwamba inalifanyia kazi suala hili kuweka katika mazingira ya usafi na kulinda miripuko pindipo kuna tishio la kufanya hivyo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy:

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni lini mtaandaa utaratibu kwa wizara yenu kuhakikisha hili suala la watu wanaojisaidia haja ndogo au kubwa sehemu ambazo hazitakikani, mkaandaa mfumo mtu yeyote au raia yeyote anaweza akamkamata mtu njiani atakapompeleka akapewa yeye shilingi elfu thalathini na yule aliyekamatwa atalipishwa faini ya shilingi laki moja ili suala hili lizidi kukomeshwa.

(b) Kwa kuwa mmekubali watu wanafanya haja ndogo hasa katika maeneo ya mjini, ni sehemu gani hizi za mjini ambazo mmezikamata au mtaa gani au jina gani hasa wanafanya haja ndogo sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba juhudi ambazo zimekuwa zikichukuliwa nimesema katika jibu langu la msingi, zimekuwa zikichukuliwa kwa aina tofauti ambavyo tunaona kwamba inafaa.

(a) Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi ushauri aliosema wa kwamba sasa tuandae utaratibu wa kutoa maelekezo kwamba kwa mtu yeyote ambaye ataweza kuwabaini katika maeneo ya watu ambao wanajisaidia haja ndogo katika maeneo ovyo, basi ushauri huu naomba ni vyema tuuchukue na kutokana na kwamba juhudi mbali mbali zinafanyika tokea hapo ambavyo wameuliza ni kwamba shughuli hizi ni moja katika jukumu la mabaraza yetu.

Sasa kwa mantiki hiyo katika namna ya kuboresha naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi ushauri wake ambao ameutoa tutauchukua, lakini ni lini juhudi hizi zinaendelea na ni kwa sababu ni moja katika jukumu la mabaraza yetu. Kwa hivyo, na hili la kutoa

bonus naona katika hali ambavyo tunaona kwamba inafaa tutaweza kushauriana tutakaa tuone kwamba lengo lako wewe Mhe. Mwakilishi ni kuona kwamba juhudi hizi zinazaa matunda. Kwa hivyo, na mimi nikuhakikishie kwamba ushauri huu tunauchukua na tutaufanyia kazi kuona kwamba tunapambana nayo hii hali ili isiweze kuleta madhara zaidi.

(b) Sehemu ambazo zimekuwa zikifanyika matokeo haya kwa takribani katika mji wetu wa Zanzibar, niseme kila panapo mkusanyiko wa watu mambo haya yanaweza yakajitokeza hususan pembezoni kidogo katika vituo hivyo vya daladala. Sasa ni vigumu kusema kila sehemu lakini niseme kwamba kwa ujumla kila panapomkusanyiko tabia za watu zinakuwa zinatofautiana na lolote katika maeneo hayo linaweza kutokea.

Kwa hivyo, nikwambie tu Mheshimiwa kwa kiufupi kwa ujumla ni maeneo yote yenye mkusanyiko mambo haya yanaweza yakatokea. Ahsante.

Nam 71

Ufinyu wa Afisi Wilaya ya Magharibi 'B'

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza**:**

Katika Ofisi ya Wilaya ya Magharibi 'B' tumeshuhudia ufinyu mkubwa wa nafasi kutokana na Kitengo cha Afya *D.H.M.T* kukaa pamoja na Ofisi nyengine kama ile ya Vitambulisho.

(a) Jee, ni lini sasa kitengo kile cha *D.H.M.T* kitaondoka ili kuacha Ofisi moja ijitosheleze katika Ofisi hiyo.

(b) Hatuoni kuwepo kwa ufinyu wa Ofisi ile kunapelekea kukosekana kwa nafasi kwa wafanyakazi ambapo hivi sasa wanakaa watu sita chumba kimoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye kifungu (a) na (b) lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti**,** itakumbukwa kuwa mnamo mwezi wa Disemba, 2014 Baraza lako Tukufu lilipitisha Sheria Nam. 8 ya Tawala za Mikoa, Sheria ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kurahisisha shughuli za utawala na uendeshaji wa shughuli za Serikali katika Mamlaka za Mikoa. Sambamba na hilo, mnamo mwezi wa Mei, 2015 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mamlaka aliyopewa kupitia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Toleo la 2010 katika kifungu cha 2 A aliigawa Zanzibar katika Wilaya 11 badala ya Wilaya 10 zilizokuwepo hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti**,** kufuatia ugawaji huo, iliyokuwa Wilaya ya Magharibi iligawiwa na kufanywa Wilaya mbili za Magharibi "A" na "B". Ugawaji huo umepelekea mahitaji ya Ofisi kuongezeka kutoka Ofisi moja iliyoko Mwera ambayo sasa inatumika kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A' na kuhitajika Ofisi ya pili kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B'. Kuanzia Mei, 2015 hadi Mei, 2016 Wilaya zote mbili zilitumia Ofisi moja iliyopo Mwera wakati jitihada za kutafuta Ofisi nyengine zikifanyika. Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo, Serikali ilitoa maelekezo kuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'B' ihamie katika majengo ya iliyokuwa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali yaliyopo Mwanakwerekwe, majengo ambayo baadhi ya vyumba vyake hadi sasa vinatumika kwa ajili ya Ofisi ya Kamati ya Uongozi wa Afya ya Wilaya ya Magharibi B (*District Health Management Team*). Hali hiyo imepelekea nafasi iliyobaki kutokidhi mahitaji halisi ya Ofisi ya Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 71 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Ofisi yangu kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, inaangalia uwezekano wa kuihamisha Ofisi ya *DHMT* kutoka mahali ilipo hivi sasa kwenda katika Ofisi ya Manispaa ya Magharibi 'B'. Hii ni kwa sababu sekta ya Afya ni miongoni mwa sekta ambazo baadhi ya majukumu yake yatahamishiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mpango wa Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi (D by D).

Hivyo basi, kuondoka kwa Ofisi hizi za *DHMT* kunatarajiwa kwenda sambamba na Utekelezaji wa Mpango wa Upelekaji wa Madaraka kwa wananchi mwanzoni mwa mwaka ujao wa fedha.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ofisi yangu inakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kuwa ufinyu wa ofisi ile unapelekea kukosekana kwa nafasi za kutosha kwa wafanyakazi, na hivyo kusababisha msongamano na ndio maana imekuwa ikichukua juhudi za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo kama nilivyoeleza katika majibu yangu hapo awali. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Nashukuru kwamba amekiri nafasi ile imekuwa finyu kwa Wilaya ya Magharibi B na ugawanaji kwa kutoka ofisi ya iliyokuwa ya Magharibi A na wakahamishiwa pale Magharibi B, ilitokana na kuwa uongezekaji kwa idadi ya watu. Sasa basi pale kwenye ofisi ya Magharibi B, kuna baadhi ya sehemu za ufanyaji kazi hazipo.

Kwa mfano, Kitengo cha Utambulisho, Kitengo cha Elimu, Kitengo cha Vyeti vile vile pale havipo, bado vimebakia katika sehemu ya Magharibi A, jambo ambalo wananchi wa Wilaya ile wanapata usumbufu wa kutoka asubuhi kwenda Magharibi A, labda pengine kafuatia cheti cha kuzaliwa, kutoka asubuhi mpaka pengine kakipata saa saba, lakini arudi nacho cheti kile keshakipata kule aje apige tena msongo Magharibi B kwa ajili ya kupata saini ya Mkuu wa Wilaya. Je, hatuoni kwamba kuwepo kwa kadhia hii kunapelekea wananchi kuzidi kupata usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala zima la usumbufu ambao wananchi wetu wanaendelea kupata katika maeneo ya kutafuta huduma kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Magharibi B.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, katika majibu yangu ya awali nilikiri kwamba kuwepo kwa kadhia mbali mbali ambazo miongoni mwao ameziainisha, lakini nyengine ndio ameziongezea. Nilisema kwamba tunakiri kuwa usumbufu bado upo na tulisema kwamba juhudi ambazo zinachukuliwa na wizara yetu, katika kuona kwamba ufumbuzi unapatikana ili wananchi wetu wapate huduma katika mazingira ambayo yako sawia, ni kuitoa

ofisi ile pale au kitengo kile cha *DHMT* kukipeleka katika jengo jengine ambalo ni ofisi ya Baraza la Magharibi B, ambako baadae kunaweza kukatupa nafasi ya kutosha ya kuona kwamba sehemu zile ambazo zimebakia kwa kweli pale zinaonekana wao wamechukua eneo kubwa.

Kwa sababu pale vile vile kuna *store* ambayo inahifadhiwa madawa na mambo mengine. Kwa maana hiyo pale ambapo tutawatoa wale au watatoka pale kwenda sehemu nyengine, kutatupa fursa ya kuweza kujipangia mambo vizuri, na kwa wale ambao kwa kweli taasisi au vitengo ambavyo vilihitajika viwepo pale, basi vinakuja pale katika ku-*cover* zile sehemu ambazo zimeachwa na hiki kitengo husika. Naamini baada ya kufanya hivyo, tunaweza tukaona kwamba huduma zitatoka kwa ufanisi na hakutakuwa na malalamiko ambayo yanafanana na hali kama hiyo ambayo tunaona inaibuka au inatokezea.

Kwa hivyo, nikuombe Mhe. Mwakilishi, endelea kuwa mdau, wanasihi wananchi wetu na kuona kwamba tunaendelea katika kutafuta ufumbuzi juu ya mambo haya au kadhia mbali mbali ambazo zinawakabili. Dhamira ya serikali ni kuona kwamba ufafanuzi au utekelezaji mzuri wa utoaji wa huduma unapatikana, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nawaombeni mazungumzo au maelezo yawe ni madogo madogo, kwa sababu jawabu linalotolewa hajibiwi mjumbe mmoja, tunajibiwa sote na tuweze kujua ni maelezo gani yanatolewa. Kwa hivyo, kama tunavyojua ukumbi wetu una *echo*, yule akizungumza kwa sauti matokeo yake hata katika vyombo vyetu ya habari vinaweza kuleta matatizo na tukakosa kusikia vizuri, naomba sana kwa hili. Mhe. Suleiman swali la nyongeza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuamka salama wa salimini.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwamba nawashukuru sana kwa kazi mnayoifanya, kwa sababu mji wetu wa Zanzibar ni mji mdogo au ni mji finyu kwamba nafasi yake ni ndogo. Nashukuru mmefanyakazi ya ziada kuwaondoa dada njoo, kaka njoo na kuwatafutia sehemu nzuri ambayo umewaweka. Lakini bado nimeona kwamba katika mji wetu wa Zanzibar kitovuni Darajani, kuna mnada ambao unaletwa vitu vibovu vibovu na vimeza vibovu vibovu kuja kuwekwa pale. Wale hawaingii katika sehemu ya dada njoo na baba njoo wakasogea kule, ili kutupisha nafasi kwa

sababu sioni umuhimu wao ambapo watu wengi wanapata mambo mengi ambayo yako maeneo ya kule tulikowapangia. Swali langu lina (a) na (b).

a) Je, wale wana umuhimu wa kuondoka ama wa kukaa pale,
b) Kama hawana ni lini wataondoka ili kupisha nafasi angalau mji wetu ukakaa katika mandhari nzuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Mhe. Mwakilishi arejee swali lake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman rudia swali lako.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nazungumza kwamba Ofisi yetu hii ambayo imefanyakazi nzuri sana ya kuwaondoa au kutoa nafasi sana ya wale dada njoo, kaka njoo ambao walikuwa wamejazana katika mji wetu wa Zanzibar hasa Darajani, na wakatafutiwa sehemu ya Maruhubi kwenda kukaa kule, ambako ndio nafasi kubwa ambako inafanyika biashara hiyo. Lakini nikiangalia kuna kitendo kimoja cha mnada ambacho kiko pale Darajani kinafanyika na kitendo kile kikifanyika siku ya mnada inakuwa fujo kubwa sana, na ninavyofikiria kwamba mnada huwa unakusanya watu wengi ambapo nafikiria kwa wakati huu wamehamia kule maeneo ambayo wamepangiwa wale watu.

(a) Je, kuna umuhimu wa kitendo kile bado kubakia pale au hakuna.
(b) Lakini kama hakuna ni lini wataondoka?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la msongomano ambao unakuwepo katika kipindi cha mnada ambao unafanyika katika maeneo ya mjini na kuona kwamba kama kuna umuhimu wa kuondoka ama kutokuwa na umuhimu wa kuondoka, na kama ni kuondoka ni lini hatua zitachukuliwa katika kuona hao watu wanaondoshwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuambie Mhe. Mwakilishi kwamba kama nilivyotangulia kueleza katika majibu katika swali namba 45. Moja katika mkakati ambao Ofisi yangu unao ni kuhakikisha kwamba mji wa Zanzibar unakuwepo katika hali ya usafi na kuwepo na haiba nzuri ya kupendezesha ili kuona kwamba tunapunguza huo msongamano ambao hauna ulazima.

Kwa hivyo, kutokana na swali hili ni kwamba umuhimu wa kuondoka mimi niseme kwamba upo, lakini tunatizama namna gani ya kuweza kuona kwamba tunawaondosha watu wetu hawa ili kusudi kwamba lengo la serikali sio kuwakomoa wananchi, lakini bado suala la kutoa huduma bora litabakia pale pale. Kwa hivyo, cha msingi umuhimu wa kuondoka watu hao upo katika mnada maeneo yale pale, lakini hatuwezi tukasema kwamba tuanze kwa *speed*, lazima tuangalie uwezekano na ushauri ambao unatusaidia, tutashauriana ili tuone kwamba ni jinsi gani tunaweza tukalitekeleza jambo hili na tuliangalie madhara katika pande zote.

Lakini kwa suala la kwamba ni lini kuondoka, bado siwezi kutoa jibu kutokana na kwamba tunaangalia uwezekano pale tukiondosha. Utaratibu tulionao sasa hivi pale ambapo tutachukua hatua katika maeneo ambayo tunaona kwamba yana maslahi zaidi kwa nchi, tuone kwamba tunatafuta na eneo jengine mbadala, ili kuweza kuona kwamba wananchi wetu badala ya kuwapa huduma zilizo bora na sio kuwakomoa. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi ushauri wako tunauchukua. La kweli ambalo umeliona tutahakikisha kwamba ushauri tunaufanyia kazi kuona namna gani tunaweza tukautekeleza kutokana na mazingira hayo ya pande zote mbili.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 103

Utaratibu wa Upelelezi Makosa ya Udhalilishaji

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya serikali ya utekelezaji wa haki na ustawi wa mtoto ya mwaka 2015/2016 inaonesha jumla ya kesi 369 za kubakwa na kesi 15 kulawitiwa ziliripotiwa kwa Unguja, na kesi 25 za kubaka na moja ya kulawitiwa, zilizoripotiwa kwa Pemba. Kwa kuwa hivi sasa inasemekana kwamba kuna idadi kubwa sana ya matokeo hayo ambayo hayajaripotiwa kutokana na wananchi kukata tamaa ya jinsi ya mwenendo wa kesi hizo unavyokwenda, ambapo hutolewa visingizio mbali mbali, vikiwemo vya ushahidi kutokamilika jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa vitendo hivi.

a) Je, serikali haioni kwamba utaratibu uliopo hivi sasa wa kufanyika upelelezi kwanza, kunasababisha kesi kuchukua muda mwingi na kutoa nafasi kwa wahalifu kuendelea kufanya makosa kama haya na

kusababisha kufutiwa kesi kwa kukosekana ushahidi kama inavyodaiwa na Mahkama.

b) Ni lini serikali itaanzisha na kuweka utaratibu maalum wa kuziendesha kesi hizi kwa muda mfupi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 103 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba nitofautiane na maoni ya Mhe. Mwakilishi kwamba kuwepo kwa dhana ya kufanya upelelezi kwanza kunapelekea kesi kuchukua muda mrefu na kutoa nafasi kwa wahalifu kuendelea kufanya makosa au hata kesi kufutwa Mahkamani.

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ya 1984 katika Kifungu cha 12(6) (b) kinasisitiza kwamba, naomba kunukuu;

"Mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka atakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, ili mtuhumiwa atiwe hatiani kwa kosa la jinai ni lazima upande wa mashitaka uwe na ushahidi wa kutosha kuthibitisha kosa linalodaiwa. Utaratibu wa kufanya upelelezi kwanza unasaidia sana katika kubaini iwapo kosa analotuhumiwa nalo mtuhumiwa limetendeka au halijatendeka.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa sababu zinazopelekea Mahkama kufuta kesi, ni pamoja na kukosekana kwa ushahidi wa tuhuma zilizowasilishwa Mahkamani. Hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wananchi kuondoa muhali na kuwa tayari kutoa ushahidi ili Mahkama iweze kuwatia hatiani wahalifu.

b) Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha kwamba kesi zinaendeshwa kwa haraka. Miongoni mwa hatua hizo, ni pamoja na kukamilisha upelelezi kabla ya kufungua kesi mahkamani. Serikali pia imeshafanya mapitio ya sheria mbali mbali, ikiwemo Sheria ya Ushahidi ili kuondoa kasoro zilizokuwa zinakwaza

utoaji wa ushahidi, ikiwemo kutambua ushahidi wa mtoto mdogo, ushahidi wa kidigitali pamoja na kukubalika kwa ushahidi wa watu wa makundi maalum.

Aidha, wizara kwa kushirikiana na Mahkama, imo katika hatua za mwisho za kukamilisha utaratibu wa kuendesha kesi, kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yaani (*case management system*), ili kurahisisha uendeshaji wa kesi Mahkamani.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mhe. Naibu Waziri, lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sheria ya kumuweka mtu mahabusu ni ya muda maalum, kama hivyo ndivyo namuomba Mhe. Waziri aniambie ni asilimia ngapi ya makosa hayo ambayo kesi zake zimekwisha, kwa wastani angalau wa mwezi, miezi mitatu au minne toka mtu kupelekwa Mahakamani na kutiwa hatiani kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 mpaka leo.

b) Je, ni sababu gani hasa za msingi zinazopelekea au kulazimisha utaratibu huu wa kesi wa upelelezi kwanza, na tukaachana na utaratibu wetu wa zamani ambao tulikuwa tunautumia hasa kwa makosa makubwa kama haya ya kudhalilisha na kulawiti kijinsia, pamoja na wanawake na watoto. Naomba majibu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na asilimia ngapi ya hizo kesi, kutoka mwaka 2015 hadi hivi sasa, naomba swali hili nimjibu kwa maandishi.

b) Sababu za msingi ambazo zinapelekea kufanywa upelelezi kwanza ni kwamba kama nilivyojibu katika swali mama, nilinukuu hapa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, katika kifungu cha 12(6)(b), naomba kunukuu tena;

"12(6)(b) Mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai, hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka atakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo".

Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike kwamba sheria zote zilizokuwepo nchini zipo chini ya Katiba. Kwa hivyo, kama sisi

tutatoa dhana hii ya kwamba kesi ziendeshwe bila ya kufanyiwa upelelezi, tutakuwa tunakwenda kinyume na Katiba. Kwa hivyo, hiyo ni sababu ya msingi kwamba upelelezi unafanywa kwanza kabla ya mambo mengine, kutokana na Katiba yetu ambayo inatusimamia.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa imebainika kuwa kesi nyingi za watuhumiwa wa makosa ya udhalilishaji na ubakaji sio watoto, na miongoni mwa wanaofanyiwa kesi hizo ni watoto.

Je, serikali haioni kuwa ipo haja ya kuanzisha Mahakama maalum kwa ajili ya makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa suala la kuanzishwa Mahakama ya Watoto katika kushughulikia masuala ya watoto ni muhimu sana. Lakini naomba Mhe. Mjumbe ufahamu kwamba hivi karibuni ilifunguliwa Mahakama ya Watoto kule Mahonda. Kwa hivyo, hizo ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo yanafanyika katika kulipigia kelele suala hili la udhalilishaji wa watoto.

UTARATIBU

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri hakunifahamu. Nafahamu kwamba Mahakama ya Watoto ipo, hili ninalosema mimi ni Mahakama Maalum, ile ni ya watoto na wanaohusika na haya makosa ya udhalilishaji sio watoto. Suala langu mimi ni kwamba Mahakama Maalum kwa ajili ya udhalilishaji na ulawiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, makofi yanafanya hata hapa Mhe. Naibu Waziri alikose hilo swali lenyewe. Kwa hivyo, mpeni utulivu. Mhe. Zulfa Mmaka muulize tena Mhe. Naibu Waziri ili uweze kupata jibu lako.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Rais, ninafahamu kwamba kuna Mahakama Maalum kwa ajili ya Watoto, ila naamini kwamba swali langu hukulifahamu. Mimi ninaloomba ni kwamba Mahakama Maalum kwa ajili ya kesi ya ubakaji na udhalilishaji wa kijinsia, sio Mahakama ya Watoto, Mahakama Maalum kwa kesi za udhalilishaji na ubakaji wa jinsia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, unapozungumzia Mahakama Maalum ya

kushughulikia masuala ya watoto na tunapozungumzia Mahakama ya Watoto vitu hivi naona havina tofauti kubwa, lakini nimwambie Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwamba Serikali kama wewe ni shahidi wa hayo imekuwa ikipiga hatua siku hadi siku kuhakikisha kwamba watoto haki zao zinaendelezwa kulindwa.

Hivi sasa tayari tumeshafungua hiyo Mahakama ya Watoto na hii Mahakama ya Watoto ambayo iko Mahonda hii inakuwa kwa ajili ya watoto. Sasa unapozungumzia kuwa Mahakama Maalum kwa ajili ya Watoto naona na hii Mahakama kwa ajili ya Watoto, lakini sasa kama unahisi upo umuhimu wa kuwekwa hiyo Mahakama Maalum kwa ajili ya Watoto basi tutaliangalia na iwapo hali itakaporuhusu tutaweka hiyo Mahakama Maalum ya Watoto. Lakini tuelewe kwamba Mahakama ya Watoto ipo Mahonda na hii kwa ajili ya watoto na sio kwa ajili ya watu wazima.

UTARATIBU

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Kifungu cha 37 Mhe. Waziri hajanifahamu hajajibu suala ambalo nimemuuliza. Mhe. Waziri naomba unijibu suala ambalo nimekuuliza sijakuuliza Mahakama ya Watoto, mimi nafahamu uwepo wa Mahakama ya Watoto, naomba unijibu swali ambalo nimekuuliza.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mhe. Mjumbe kile ambacho alikuwa akiuliza, kwanza naomba niunge mkono majibu ya Mhe. Naibu Waziri na nimpongeze.

Swali la Mhe. Mjumbe alikuwa akiulizia suala la Mahakama Maalum kwa ajili ya makosa ya udhalilishaji na mengineyo kama hayo, kimsingi mfumo wa Mahakama wa Zanzibar tuna mfumo wa Mahakama ya Kadhi ambao unahusiana na masuala ya Kiislamu, mirathi na masuala ya ndoa za Kiislamu. Upande wa pili kuna Mahakama za *Common law* na utaratibu wake kwamba tuna Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mkoa na Mahakama Kuu.

Katika upande huu wa *Common Law* kuna makosa ya aina mbili, kuna makosa ya *civil* kwa maana kwamba makosa ya madai na makosa ya jinai. Mahakama nyengine iliyoanzishwa na Serikali ni Mahakama kwa ajili ya makosa ya udhalilishaji wa watoto ambayo tunaweza tukai- *categories* kama ni hiyo Mahakama Maalum.
Swali la Mjumbe kwamba anataka kujua kwa nini kusiwe kuna Mahakama Maalum kwa ajili ya makosa haya ya udhalilishaji. Makosa ya udhalilishaji ni

sehemu ya makosa ya jinai na mfumo wetu wa Mahakama una haki, una fursa na Sheria zinalazimisha, makosa yote ya jinai kuhukumiwa katika msingi huo wa makosa ya jinai kwa upande wa Mahakama. Sasa kuwa na Mahakama Maalum katika makosa haya ya jinai kwa kushughulikia tu makosa haya ya udhalilishaji naamini kwamba hatujafika huko, bado utaratibu wa kesi katika mfumo wa kawaida kuzi-*categories* katika makosa haya ya jinai imani yangu kwamba jambo hili tukisimamia sheria zetu vizuri, Polisi wakifanya kazi zao vizuri, *DPP* akifanya kazi zake vizuri makosa haya yatapungua na pengine yataondoka kabisa.

Kwa hivyo Serikali imeona upo ulazima wa kuanzisha Mahakama kwa ajili ya kulinda haki za watoto na hiyo ndio tunaweza tukasema kwamba Mahakama Maalum kwa ajili ya kulinda watoto, kwa maana kwamba ni *Juvenile Court* na madhumuni makubwa ni kuona mazingira ya mtoto namna anavyoweza kutoa ushahidi anatofautiana na mtu mzima, kuna utaratibu unaokwenda *in camera*, taratibu za kukaa *open,* lakini unamlinda yule mtoto aweze kutoa ushahidi kwa yale mazingira yake. Kwa mtu mzima akitendewa kosa la udhalilishaji au jengine lolote tunahesabu kwamba hilo ni kosa la jinai na anapata fursa ya kutoa ushahidi wake katika Mahakama kwa mujibu wa utaratibu na mfumo mzima wa Mahakama ya Zanzibar.

UTARATIBU

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 37 kinataka Mhe. Waziri au mjumbe yeyote anaweza kuuliza swali ambalo madaraka yake ajibu kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, swali lilikuwa Mhe. Mjumbe anaiomba Serikali kuanzisha Mahakama Maalum inayoweza kusikiliza makosa haya ya udhalilishaji, tumeshuhudia sote Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameanzisha Mahakama ya Mafisadi ameiomba ipo, Zanzibar tunayo Mahakama ya Ardhi ipo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa hapa ni kutaka Serikali ianzishe Mahakama Maalum kutokana na huu udhalilishaji umezidi Zanzibar, umezidi na unaendelea kila siku. Hilo ndilo lilikuwa swali la msingi na ilikuwa haina haja ya kwenda Kusini wala Kaskazini ni ombi la kuanzishwa kwa Mahakama Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibiwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu wa kawaida kabisa kwamba

tunakuja hapa kwa madhumuni ya kutaka kuendeleza nchi yetu kwa maslahi ya wananchi wetu, nilikuwa namsikiliza Mhe. Mjumbe alipokuwa anazungumzia utaratibu nilitegemea labda kuna jambo ambalo tumekwenda kinyume na utaratibu. Suala la Baraza kuiomba Serikali ni kitu cha kawaida na Serikali ku-*respond* ni wajibu wetu.

Tulichokisema kwamba kosa hili la udhalilishaji ni sehemu ya makosa ya jinai na imani yetu kwamba sheria zetu zinakidhi na kuweza kusimamia, hatujakataa kwamba Rais wa Jamhuri hajaanzisha Mahakama ya Mafisadi, mazingira na mahitaji yalilazimisha kufanya hivyo, sisi tunadhani sasa hivi Serikali tatizo hili lipo lakini kwa namna ambavyo tunaamini tukivipanga vyombo vyetu vikiwajibika ipasavyo kosa hili litapungua na litaondoka. Hatuna sababu ya kulazimisha kwamba jambo hili tulifanye leo kwa sababu limefika hapana, jambo lipo lakini imani yetu ni kwamba Sheria zinakidhi na tunaweza kuanzisha hilo jambo ikifika wakati, hivi sasa kama kila mmoja atawajibika na sisi ni sehemu ya jamii na sisi ndio hao tunaokwenda kuzungumza katika kupotosha hili jambo katika sehemu husika wamo baadhi ya viongozi yanatokea masuala haya wanakwenda Polisi, wanashiriki katika kuomba msaada Polisi wanapotosha, wanaupunguza ushahidi wanakwenda kwa *DPP* haya yapo niseme.

Kwa hivyo tunachokisema sisi kwamba bado makosa haya yapo lakini mfumo na utaratibu wa kisheria tunao uwezo wa kuyashughulikia kuyapunguza na ikibidi kuyaondosha kabisa, na kama kutakuwa kuna ulazima wa kuanzisha Mahakama hiyo Serikali haichelewi na tutaanzisha. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Hili ameshalitolea maelezo vizuri na Serikali imeshalisikia.*(Makofi)*

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kesi za udhalilishaji zinaongezeka siku hadi siku kitendo ambacho kinaitia aibu nchi yetu na kwa kuwa kesi hizi si miongoni mwa kesi zinazochukuliwa dhamana, kitendo ambacho huvuruga ushahidi.

a) Je, Wizara haioni sasa umefika wakati wa makosa haya ya udhalilishaji yawe ni miongoni mwa kakosa yasiyochukuliwa dhamana.

b) Serikali haioni kuwa sasa ipo haja ya kuongeza kiwango cha adhabu kwa watu wanoahusika na makosa hayo kwa sababu kiwango cha hivi sasa ni kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa masuala ya udhalilishaji ni mambo ambayo yanatuumiza moyo, hayatupi raha masuala ambayo kila tukilala na tukiamka tukisikia masuala haya yanatokezea kwa kweli hayatupi furaha. Ushahidi wa hayo hata Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba zake nyingi hususan zile ambazo alipokuwa akifungua mahakama ya watoto, au hata siku ile ya Sheria Zanzbar. Kama Waheshimiwa Wawakilishi mlikuwa mnafuatilia sana na mko makini zaidi katika ile hotuba yake pale ambapo nimesikia kwa kweli anazungumza katika nguvu zake za mwisho kuona kwamba hili suala limemtosha.

Kwa kiwango fulani unaona kama amevunjika moyo lakini bado hajakata tamaa, sasa niungane na wewe Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli suala la udhalilishaji ni suala ambalo zito na linatunyima raha.

Sasa kuhusiana na masuala ya dhamana ni kweli kwa sababu tayari imeshafikia hatua kubwa sana na mbaya sana kwa masuala ya udhalilishaji Zanzibar kwa hivyo ni vyema tukahakikisha kwamba suala hili nalo tukaliangalia sheria zaetu nalo tukaliweka katika sehemu kama hiyo ambayo ya kutopatiwa dhamana. Kwa hivyo nimwambie tu hali hii ni kweli ipo na upo uwezekano wakati wowote na hili tukaliweka miongoni mwa hayo makosa wasiyopatiwa dhamana ili kuhakikisha kwamba tunalinda zaidi heshima yetu ya Kizanzibari kuhusu haya masuala ya udhalilishaji.

Suala la pili, kwa kuwa suala hili ni zito na limekuwa likitukera kama nilivyozungumza awali adhabu ambayo ipo kama ni ndogo basi ni vyema adhabu hii iongezwe. Kwa sababu adhabu hii iliyokuwepo kama tutaiongeza bila ya shaka hawa wote ambao wana tabia hizi za udhalilishaji wanaweza wakakoma na tukawa tunaishi vizuri katika Zanzibari yetu bila ya kuwa na udhalilishaji wa aina yoyote.

Nam 67

Uharibifu wa Mazingira Eneo la Hifadhi Maruhubi

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:-

Eneo la Maruhubi ni moja ya sehemu za Kihistoria kwa nchi yetu ya Zanzibar. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa vitendo vinavyoathiri haiba nzuri ya eneo hilo na vikiwemo vitendo vya ukataji miembe, minazi na miti mengine.

a) Je, Serikali haioni kwamba ukataji huo wa miti unaondoa haiba nzuri ya eneo hilo na kuharibu mazingira.

b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliendeleza eneo hilo la Maruhubi.

c) Pamoja na lengo zuri la kujenga ukuta katika eneo hilo, lakini bado wapo watu wanaamua kuruka ukuta huo, ni hatua gani zinachukuliwa kukabiliana na vitendo hivyo viovu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, Kwa idhini napenda kumjibu Mheshimwia swali lake nambari 67 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekitia**,** Maeneo yote yaliyotajwa na Wajumbe yamo kwenye orodha ya maeneo yanayohifadhiwa kisheria na Serikali na yapo chini ya uangalizi wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Ni kweli kuna ukataji wa Miembe na Minazi katika eneo la Maruhubi na hali hiyo inaondowa haiba ya asili ya eneo hilo. Lakini miti hiyo hukatwa kwa sababu mbili kubwa, nazo ni:

Kukauka na kuanguka kwa Miembe na Minazi hiyo.

a) Miembe na Minazi hiyo huwa tayari imekauka na baadhi ya wakati husababisha maafa kwa watu waliokaribu na maeneo hayo. Aidha wananchi waliopo kwenye eneo huiomba pindipo ikitokea hali hiyo na Idara huwauzia kwa kuomba kibali Idara ya Misitu na Mali zisizorejesheka kwa hatua ya ukataji pale watakapo thibitisha ukweli wa ombi lao.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mikakati kadhaa ya kuliendelea na kulifanya eneo la Maruhubi kuwa kivutio kikubwa cha wageni. Kwa kuliona hilo Wizara Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imefanya yafuatayo:-

Kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Tawala za Mikoa na Idara Maalum, imeweka ulinzi wa kudumu katika eneo hilo kwa ajili ya kuweka usalama wa wageni na mali zao

Mhe. Mwenyekiti**,** Serikali tayari imeshalipima eneo hilo la Maruhubi na kupeleka maombi ya kupatiwa hatimiliki kwa ajili ya kudhibiti eneo hilo. Serikali inampango wa kupanda miti ya ziada ili eneo hilo liendelee kuvutia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Idara yake ya Makumbusho na Mambo ya Kale inatayarisha vipindi vya Redio na Televisheni kwa ajili ya kuyatangaza maeneo hayo na kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa maeneo ya kihistoria likiwemo eneo la Maruhubi.

Mhe. Mwenyekiti, Vile vile Serikali kwa kushirikiana na jamii wameweka ulinzi shirikishi katika eneo la Maruhubi kwa ajili ya kulinda rasilimali hiyo. Aidha Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na baadhi ya Taasisi za kiraia na wafanyabiashara ndogo ndogo kwa kulitumia eneo la Maruhubi kwa biashara za bidhaa za kitalii, lakini vile vile kuangalia uwezekano wa kuifanya Maruhubi kuwa kituo cha Mapumziko na kupunguza msongamano wa watu katika eneo la Forodhani.

Mhe. Mwenyekiti, Ni kweli kuna watu wachache wanaoruka ukuta na kuingia ndani ya eneo hilo, lakini kwa kushirikiana na jamii (Kikundi cha Uhifadhi cha Maruhubi) hali ya hiyo imepunguwa sana na kupunguza wimbi la uharibifu wa eneo hilo kama kuchimba mchanga n.k.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti hata hivyo bado wapo watu amao wanaendelea kubomoa na kuruka ukuta, lakini juu ya hivyo pia wanaendelea kuharibu kuna mazao pale kama miembe.

a) Je, Mhe. Waziri Wizara yake kwa sababu kuna askari pale mlangoni wamewekwa, anaonaje wale askari badala ya kuwatumia

mlangoni wakenda kufanya doria katika mazingira ya ule ukuta ili pasiasirike.

b) Ni lini ataweza kufanya hayo maendelezo kwenye hiyo sehemu ili wananchi wa eneo lile wapate tija na kupata maendeleo katika eneo lile la Maruhubi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mjumbe swali lake kama ifuatvyo:

(a) Ni kweli kwamba pale tuna askari mlangoni na uhalifu wakati mwengine wahalifu hawaji wakati wa mchana, wahalifu wa aina hii ambao wamekusudia lengo lao kuharibu maeneo haya pamoja na kuwepo ulinzi pale mlangoni wanakuwa wanaingia wakati wa usiku, lakini hata hivyo Wizara bado inashirikiana na vikosi hivi wakati mwengine wanakuwa wanafanya doria, na huu uingiaji usiku kwa wale waharibu umepungua sana na tunahakikisha kwamba utaondoka zaidi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali mama lini utaratibu huu wa kuliendeleza utaanza tumo katika mpango maalum wa matayarisho haya, kama nilivyoeleza kwamba tutahakikisha kwamba eneo lile limeboreka wageni na watalii kitakuwa ni kituo cha mapumziko.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri Mhe. Machano Othman Said swali la nyongeza.

Mhe. Machano Othman Said:

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika miaka ya 2005 mpaka 2010 wakati eneo lile liko chini ya Wizara ya Elimu, Utamaduni na Mhe. Waziri alikuwa ni Mhe. Haroun Ali Suleiman wananchi wa Wadi ya Muembe Makumbi waliomba kwa kupitia mradi wa *TASAF* kupewa eneo lile na walianza kuyatengeneza yale mahodhi ya Maruhubi. Je, ombi lile lilifikia wapi.

(b) Inasemekana kwamba pamoja na wingi wa miembe katika eneo la Maruhubi wakati wa kukodisha miembe ile huwa unakodishwa muembe mmoja tu. Lakini huyo anaekodi anachuma miembe kuliko kumi au kumi na tano. Je, suala hili lina ukweli gani na serikali

inachukuwa hatua gani kulimaliza tatizo hili ili serikali iweze kupata mapato.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, samahani naomba arejee swali lake sikumsikia.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, swali la kwanza au yote mawili.

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika miaka ya 2005 hadi 2010 wananchi wa Muembe Makumbi wakiongozwa na Mwakilishi wao walianzisha ushirika ambao ulianza kufanya matengenezo ya Mahodhi ya Maruhubi na kuiomba serikali iwape wao waendeshe ili kupijipatia kipato lakini pia kulinda mazingira na usalama wa eneo la Maruhubi. Je, hatua ule ilifikia wapi.

(b) Zipo tetesi za ukweli kwamba wakati wa ukodishaji wa miembe ya Maruhubi na maeneo mengine kwa wajanja wachache serikalini kwa kushirikiana na wakodishwaji miembe yote hukodishwa mtu kwa muembe mmoja ili atembee na risiti na kuchuma miembe yote. Je, serikali ina mpango gani wa kuzuia udanganyifu huu ambao unainyima serikali mapato.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na ushirika ambao uliomba kuendeleza eneo la Maruhubi na bado serikali inatafakari kuona suala hili ni vipi tunaweza kushirikiana na wenzetu hawa ili kuendeleza eneo hilo. Lakini la msingi ni kwamba sasa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kuwa eneo lile serikali inachukuwa hatua ya kuliimarisha na Mhe. Machano Othman Said ni shahidi kwa kuona namna gani tulikarabati ule ukuta na mambo mengine ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyasema hatua zake zimeanza na zitaendelea kuimarishwa ili eneo hilo libakie na haiba na lizidi kuvutia.

Lakini kwa kuwa kikundi chetu chetu hichi ni vizuri tutamshauri Mhe. Waziri muhusika aweze kulifikiria jambo hili na kuona ni utaratibu gani ni mzuri utakaowezesha kuendeleza eneo hili.

Kuhusu suala la mapato ya ukodishwaji miembe jambo hili tunalipokea kama ushauri ili kuhakikisha kwamba mapato ya serikali hayapotei isiwe kukodisha muembe mmoja ikachumwa kumi na moja au miembe yote kwa msingi huo ushauri huo tunaopokea na tunaufanyia kazi ili kuhakikisha mapato ya serikali yanaenda vizuri na namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake hili.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, tunafahamu kwamba sehemu nyingi za historia ndani ya mji wetu wa Zanzibar nyingi ziko karibu na bahari ikiwemo sehemu ya Maruhubi na sehemu ya Mtoni na kwengine kama Mangapwani pia na Fukuchani. Lakini pia kuna sehemu ambazo ziko juu kama Kijichi, Kizimbani na Miwani. Lakini kwa kuzungatia kwamba sehemu ambazo ziko katika fukwe yaani zimepakana na bahari ikiwemo Maruhubi na mtoni tunafahamu kwamba hizi sehemu zote zitakuwa zinahusika na sehemu ya Makumbusho.

(a) Kwa kuyaenzi makumbusho haya pamoja na fukwe zake serikali imechukua hatua gani ya kuzilinda fukwe hizi zilizopakana na haya majengo ya Makumbusho na kuwaondoa wale watu ambao tayari wameshakuwa wanazinyemelea hizi fukwe kwa kufanya mambo yao ya kihoteli na kuzitumia kama ni *beach* ambazo ziko kwenye mahoteli.

(b) Katika hizi ambazo ziko juu kama Kizimbani pamoja na Kijichi pamoja na Miwani hizi ni sehemu ambazo sasa hivi kiufupi zimesahaulikana lakini kuna watu ambao wanazitumia kwa mambo yao kwa kuwaonesha watalii na kuweza kujihudumia wao na si serikali. Jee, serikali imechukua hatua gani nao kuziona sehemu hizi za kihistoria kwa kuweza kuongeza pato la serikali na si kwa mtu binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Hidaya swali la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Ni kweli sehemu au maeneo aliyoyataja Mhe. Hidaya kwamba yamo katika maeneo ya fukwe. Lakini hata hivyo serikali hatua ambazo imekuwa ikizichukua katika maeneo haya ya fukwe kwa ajili ya historia kama Fukuchani na kwengineko. Kwa upande wa serikali imehakikisha kwamba maeneo haya kwa kuonekana tumeyatunza zaidi na kuendeleza basi kuna wale wawekezaji ambao wanakuja kuziomba sehemu hizi, kwani

wawekezaji mara nyingi wanataka maeneo ya fukwe. Kwa hivyo, serikali imekuwa ikichukua maombi yao na kuyapokea na kuyafanyia kazi hatma yake hupewa wawekezaji na kuendeleza maeneo haya na hatma yake fukwe zile hutumika maeneo vizuri na maeneo ya historia.

(b) Mhe. Mwenyekiti, sehemu hizi za juu pia maeneo ambayo ya kihistoria yako sehemu za juu pia serikali wakati wanapoingia wageni wanaendeleza kwa sababu wageni wapita maeneo yale ya kihistoria na kuyatembelea. Kwa hivyo, maeneo haya bado yanaendelea kutunzwa na wakati mwengine wafanyakazi wetu wanakuwepo pale na tunawapeleka kwa ajili ya kusafisha maeneo yale na kuyawekea mazingira mazuri ili kuonekana maeneo yale yako katika hali ya mazingira mazuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza ya Mhe. Hidaya kama ifuatavyo yenye (a) na (b) kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli serikali inaona umuhimu wa kutunza maeneo yetu ya historia na ndio maana maeneo yote ya historia yametangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali na yanalindwa na Sheria iliyowekwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Kwa msingi huo hatua mbali mbali zimechukuliwa licha ya kupata kuhifadhiwa kwa sheria na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali umewekwa utaratibu wa kuyaimarisha maeneo hayo ya kihistoria pamoja na kuweka utaratibu maalum kwa vyanzo vya mapato pale ambapo wageni mbali mbali wanatembelea sehemu hiyo.

Kwa msingi huo serikali itaendelea kuzidi kuendeleza maeneo hayo ya kihistoria kwa Sheria iliyopo pamoja na kuyasimamia yaweze kutoa mapato kama ambavyo inafanyika.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa majibu ya ziada. Swali linaendelea katika Wizara hiyo ya Habari la Mhe. Shehe Hamad Mattar litaulizwa na Mhe.Mwanaasha Khamis Juma.

Nam 110

Ving'amuzi vyote kuonesha *Channel* ya *ZBC*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kny: Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar) - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa kupata taarifa zinazohusu mambo yanayotokea ndani na nje ya nchi yetu wakati wowote kwa mwananchi ni haki yake kwa mujibu wa kifungu cha18(2) cha Katiba ya Zanzibar, na kwa kuwa Waziri alishatoa tangazo kwa vyombo vyote vya Habari Zanzibar vinavyomiliki ving'amuzi kwamba ni lazima televisheni ya *ZBC* ionekane kwa muda wote kwa kila anaemiliki king'amuzi ikiwa amelipia au hajalipa king'amuzi hicho, kama vile inavyoonekana *TBC* katika ving'amuzi vyote nchini.

(a) Je, sababu zipi zinazopelekea king'amuzi cha *AZAM TV* ikiwa hujalipia channel ya *ZBC* haionekani isipokuwa *TBC* na nyenginezo.

(b) Je, huoni kuwa hii ni kuleta dharau kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo wewe Mhe. Waziri ndie dhamana wa vyombo vya habari hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa ratiba niwekewa swali namba 67 tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, majibu.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo napenda kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake nambari 110 kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sikupata taarifa inahusu mambo yanayotokea ndani na nje ya nchi yetu wakati wowote kwa wananchi ni haki kwa mujibu wa kifungu cha 18(2) cha Katiba ya Zanzibar na kwa kuwa Waziri ameshatoa tanganzo kwa vyombo vyote vya habari Zanzibar vinavyomiliki ving'amuzi kwamba ni lazima *station* ya *ZBC* ionekane kwa muda wote kwa kila anayemiliki king'amuzi ikiwa amelipia au hajalipia king'amuzi hicho, kama vile inavyoonekana *TBC* katika ving'amuzi vyote nchini.

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba *channel* za *ZBC TV* haionekani katika king'amuzi cha *AZAM TV* ikiwa mwenye king'amuzi hicho ameshindwa kulipia ada ya mwezi. Hii ni kukosekana kwa taratibu za kiufundi ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti**,** Hata hivyo, hatua zimekuwa zikichukuliwa hivi sasa wakati ambapo *studio* za *ZBC Karume House* zikiendelea kuimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo makubwa ili kurahisisha ufikishaji wa idhaa ya *ZBC TV* kwenye mitambo ya *AZAM TV* iliyopo Dar es Salaam.

b) Mhe. Mwenyekiti, kutoonekana muda wote kwa idhaa ya televisheni ya *ZBC* katika king'amuzi cha *AZAM TV* haioneshi kuleta dharau kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wala kwa Mhe. Waziri mwenye dhaman ya habari hapa Zanzibar, badala yake ni kukosekana kwa taratibu za kiufundi ambazo bado zinaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuhakikishia Mheshimiwa kwamba Kampuni ya *AZAM TV* na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo zina mashirikiano mazuri na zimekuwa zikifanya kazi pamoja katika mambo mbali mbali na hivi sasa hatua mbali mbali za kuimarisha *studio* yetu zinaendelea ili *TV* yetu iweze kuonekana vizuri na kwa ufasaha zaidi na itakuwa moja katika *TV* za mfano katika Afrika Mashariki. Ahsante sana.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Je, ni lini hili tatizo la kiufundi au la taratibu la kiufundi limeanza.

(b) Tokea kutolewa tangazo hili kupitia chombo hichi hapa cha Baraza la Wawakilishi huu ni karibu mwezi wa tisa. Je, ni lini tatizo hili litamalizika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwanaasha kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kazi kabambe imeanza ya kufanya ukarabati mkubwa wa *studio* zetu na kama unavyojua tumeagiza mitambi mipya ya *Digital* na vile vile sasa hivi kuna utaratibu nzuri ambao utatumia ving'amuzi vya *ZBC* vitakavyowezesha kuonekana vizuri. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na Wawakilishi wengine na wananchi wote wawe na subra kwa muda huu ambao matengenezo yanafanywa ili tatizo hili la kiufundi limalizike na *TV* yetu iweze kuonekana vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuniona na kunipa nafasi hiyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa kusema kwamba *AZAM TV* na *ZBC* wana mawasiliano mazuri sana kusaidia katika masuala mbali mbali.

Jee, kwa nini *ZBC* kama wana maelewano mazuri na *AZAM TV* wasiweze kuonesha moja kwa moja mashindano ya kombe la Mapinduzi ambayo yalikuwa yanarushwa na *channel* za *AZAM TV*.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Abdalla Maulid Diwani kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikiri tena kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba yapo maelewano mazuri kati ya *AZAM TV* na *ZBC* na kwa muda ule wa Kombe la *Mapinduzi Cup* hawakuweza kushirikiana si kwa sababu ya mashirikiano mazuri yaliopo. Lakini kwa sababu za kiufundi ambazo wakati huo zilikuwa zimejitokeza na kama nilivyosema hivi sasa tunafanya ukarabati mkubwa wa *studio* zetu hapo baadae utaona namna gani *TV* hizi mbili zilivyokuwa na nia njema ya kushirikiana ili mambo kama hayo yanapotokea ni mambo ya mazungumzo na wanaelewana na watafanya vile watakavyoona inafaa kwa mujibu wa kuwafurahisha wananchi wetu.

Lakini jambo la msingi hapa ni kukamilisha na haya matengenezo yanayoendelea. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa kuna tangazo muhimu hapa kidogo. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria anawatangazia Wajumbe wakutane katika muda huu hivi sasa katika ukumbi wa Kamati, muda huu. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuuliza Mhe. Waziri kwamba:-

a) Katika miaka ya 72 ambayo tulikuwa tuna *analogy* huko lakini *TV* ya *TVZ* ilikuwa ikionekana Zanzibar na Bara kwa wakati wowote na *time* yoyote ukifungua. Tumepiga hatua katika miaka karibu 35 tuko katika *Digital, TVZ* bado viwango vyake haijafikia hiyo ya miaka 72. Ni tatizo gani ambalo limetufika mpaka ikiwa *TVZ* mpaka itumie mitambo mengine bila ya kuonekana *live* katika muda wowote ambacho ni chombo muhimu ambacho kilichokuwa hakina ubabaishaji.

(b) Kwa nini kama *ITV* na vyombo vyengine vikifika wakati fulani baada ya taarifa ya habari vinatoa wosia kama wa baba wa taifa. Je, *TVZ* kwa nini imeshindwa kutoa wosia wa Rais wetu wa kwanza wa Zanzibar.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Sarahan Said kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, atakumbuka Mhe. Mwakilishi kwamba huko nyuma mitambo yetu ilikuwa chakavu imeharibika na kwa msingi huo serikali ikafanya maamuzi ya makusudi kununua mitambo mipya ya *Digital*. Baada ya kununua mitambo mipya ya *Digital* ilionekana pia upo umuhimu wa kukarabati *studio* zetu ziweze kuendana na uwezo wa mitambo ile iliyonunuliwa.

Kwa hivyo, ndio maana sasa hivi kunatokea ukarabati mkubwa kwa *studio* zetu hizi ili ziendane na uwezo mkubwa wa mitambo ambayo ipo. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi wote kwamba mara itakapokamilika kazi hiyo basi na *TV* yetu ya *ZBC* itakuwa moja katika *TV* za mfano katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Naomba nimtoe wasi wasi sana na ataona *TV* nzuri na wananchi watapata kuona vizuri.

b) Kuhusu wosia wa Baba wa Taifa unatolewa kwenye vyombo vya *TV* kwa upande wa Tanzania Bara, ushauri wake tunauchukua ili nao wosia wa Mzee Karume uweze kutoka na nyote ni mashahidi inapokaribia wakati wa Sherehe za Mapinduzi kuna hotuba mbali mbali za Mheshimiwa Marehemu Baba wa Taifa kwa upande wa Zanzibar Mzee Abeid Aman Karume, hotuba zake zinatolewa na sote tunapozisikia hizo huwa tunaridhika sana na huwa tunaona ni maelezo

ya kiendelevu licha ya kutolewa miaka mingi nyuma huku. Lakini utaona bado maelezo yake yako hai.

Kwa hivyo, kwa ushauri huo tunauchukua, ushauri mzuri tutawasiliana na wahusika ili tupate wosia wa Mzee Karume katika *ZBC* Zanzibar.

Nam. 62

Kuezekwa Skuli ya Mgambo – Kiwengwa

Mhe. Asha Abdalla Mussa - Aliuliza:-

Sera ya Elimu inasisitiza wazazi waanzishe ujenzi wa majengo ya skuli na inapofikia hatua ya kuezeka iachiwe Wizara. Hata hivyo, kuna majengo mengi yameshajengwa Unguja na Pemba ambayo yamefikia hatua hiyo, ikiwemo skuli ya Mgambo ndani ya Jimbo la Kiwengwa ambayo bado haijaezekwa.

a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha majengo hayo yanamalizwa.

b) Je, Wizara haioni kuwa majengo hayo kukaa muda mrefu bila kuezekwa yanasababisha wanafunzi kukosa kuyatumia na kurejesha nyuma maendeleo ya elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 62 lenye sehemu (a) na (b).

a) Ni kweli Wizara imechukua dhamana ya kukamilisha majengo ya Skuli yaliyoanzishwa na Wananchi mara tu yanapofikia hatua ya kuezekwa. Kwa sasa kuna jumla ya madarasa 285 yakiwemo ya Skuli hiyo ya Mgambo ambayo yamefikia kiwango cha kuezekwa na yanahitaji kukamilishwa. Idadi hii ni kubwa kwa kukamilishwa kwa awamu moja na hivyo kukamilishwa kwa awamu mbali mbali kupitia mchango wa Serikali na kwa mashirikiano na mashirika mbali mbali wa maendeleo yakiwemo *SIDA* na *"Milele Zanzibar Foundation – MZF".* Aidha, kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, Serikali pekee imeshakamilisha madarasa 31 Unguja na Pemba pia madarasa 30 yamekamilishwa na *"Milele Zanzibar Foundation* na hivyo kubakiwa na idadi hiyo ya madarasa 285. Tutaendelea kuyakamilisha

madarasa hayo katika awamu mbali mbali zijazo kwa kadri hali ya fedha itavyoruhusu na michango mbali mbali ya washirika wa maendeleo.

b) Ni kweli na Serikali haipendelei kabisa kuona majengo hayo yanakaa muda mrefu bila ya kukamilishwa. Serikali kwa kuona umuhimu wa maendeleo ya elimu inatilia mkazo sana katika kukamilisha majengo pale tu inapopatikana fedha. Ahsante.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri tumeshuhudia kuwepo kwa majengo mengi ambayo yamekaa kwa muda mrefu na yanatokea athari ya kuporomoka kwa majengo yale lakini niseme kwamba je Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba madarasa hayo 285 kwa hatua ya mwanzo yaweze kuwezekwa ili isitokee kusababishwa na athari hizo.

(b) Wizara ina mpango gani wa ziada wa kuweza kuwasaidia wanafunzi wa Skuli ya Mgambo wakati wa mvua kwani sasa wanasoma katika hali ambayo hairidhishi chini ya miti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa sasa yamebakia madarasa kama 285 kama tulivyosema na hizi ni juhudi kubwa kabisa zilizofanywa na Wizara ya Elimu katika miaka 2 iliyopita yalikuwa madarasa haya 501. Lakini mpaka kufikia mwaka huu yamebakia 285. Kwa hivyo hizi ni juhudi zinaendelea na juhudi hizi tunazifanya kwa pamoja, Serikali pamoja na washirika wa maendeleo na katika suala hili hasa *SIDA* pamoja na *Milele Zanzibar Foundation.*

Lakini pia nataka nifafanue zaidi kwamba hayo ni madarasa ambayo tumeyakamilisha kupitia fedha za Wizara pamoja na *Milele Zanzibar Foundation*. Lakini pia Wizara kwa namna nyengine inapotokea dharura huwa tunafanya kuzikarabati baadhi ya Skuli na tunazo hapa nyingi kama 6,7, tumezikarabati na kuna nyengine inapotokea dharura kama aliyoitaja hapa Mheshimiwa hapa Skuli ya Mgambo huwa tunachukua hatua ya dharura. Kwa hivyo kwa Skuli ya Mgambo tutaiangalia na kwa kweli kama ipo haja tutachukua hatua za dharura kama tunavyotumia sehemu nyengine ili kuzikabili.

Swali (b) ni suala la Mgambo ambalo nimeshalijibu kwamba tutachukua hatua za dharura kama tunavyochukua hatua nyengine na tutafanya hivyo.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri. Mhe. Waziri Skuli ya Minungwini imekabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa madarasa ya kusomea wanafunzi wetu na hivi karibuni kuna jengo ambalo lilianguka na hivyo kupelekea changamoto kubwa ya wanafunzi kurundikana kwenye madarasa. Pamoja na changamoto hiyo ya wananfunzi kuna jengo ambalo lipo limekaa kwa muda mrefu na hadi leo hii jengo lile bado halijaezekwa. Je, Wizara yako inalijua hilo na kama Wizara yako inalijua hilo ni lini jengo lile litaezekwa ili wanafunzi wale ili kuondoshea usumbufu wanafunzi ambao wamerundikana katika madarasa ambayo yapo na hayatoshelezi. Ili kuondoshea usumbufu walimu ambao wanaupata wakati wa kufundisha wanafunzi wale.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Wizara ya Elimu inalijua tatizo la Skuli ya Minungwini, mimi binafsi nimekwenda nikaliona hali iliyo na tunaijua. Kama tulivyojibu mwanzo tutafanya kila hali inayowezekana pale ambapo tutapata ufadhili au tutapata fedha kutoka Serikalini basi suala hili la Skuli ya Minungwini nalo pia tutalishughulikia. Madarasa kama hayo kama tulivyosema yapo mengi na pale ambapo tutafanya utafiti tukaona kuna haja kubwa sana basi huchukua hatua za kukata pua na kuunga wajihi. Kwa hivyo niseme tu kwamba hali itakapokwenda zaidi tukaona kwamba kuna mahitaji makubwa zaidi juhudi za dharura zitachukuliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hatuwezi kusema lini lakini tutafanya kadri inavyowezekana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, katika ujenzi wa madarasa mbali mbali kuna ya muda mrefu, na kuna muda mfupi. Ninafikiri waratibu wa Wizara ya Elimu huwa wanafatilia katika maeneo hayo.

(a) Kwa kuwa ujenzi huo kuna majengo ambayo yamejengwa kwa muda mrefu ambayo yanakaribia kuporomoka sasa hivi Wizara inawapa kipaumbele gani ili kuyawezeka na wanafunzi wetu wakapata kusoma haraka.
(b) Kwa kuwa kuna msongomano wa watoto wengi katika baadhi ya maeneo katika hayo madarasa yaliyojengwa Wizara pia inaliangalia vipi tatizo hili ili kuondoa usumbufu kwa watoto hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

(a) kama tulivyosema kwamba Wizara na Serikali kwa kweli inaheshimu sana nguvu za wananchi katika kuchangia masuala ya elimu. Pia tunaelewa kwamba baadhi ya majengo yamejengwa katika kiwango cha chini na ndio maana yanaanza kuporomoka hata kabla hayajahamiwa hilo tunalijua. Kutokana na hali hiyo kwamba Wizara itatoa muongozo baadae wa ujenzi wa majengo haya yajengwe kwa kiwango gani na yajengwe sehemu gani. Kwa lugha nyengine sasa hivi tunafanya utafiti wa *school maping* ili wananchi tusijenge tu hivi kiholela lakini tujenge kwa mpangilio maalum wa mahitaji katika miaka mingi inayokuja.

Kwa hivyo tunaelewa suala hili na tutakapopata fedha na wahisani basi tutayaangalia zaidi haya majengo ambayo yako hali mbaya zaidi. Lakini hatutoangalia hali mbaya peke yake lakini na uhitaji, tutaangalia pia hali mbaya na uhitaji. Kwa sababu wakati mwengine kutokana na ujenzi ambao ulikuwa katika kiwango cha chini pale Wizara tunapokamilisha kwa kweli wakati mwengine inabidi tuzivunje chini tunaanza mwanzo tumefanya sehemu mbali mbali baada ya kukamilisha inabidi tuanze chini kabisa kutokana na kupungua kwa ubora wa ujenzi. Kwa hivyo tutalifanya hilo kwa kutegemea uchakavu wa majengo lakini na mahitaji ya eneo lenyewe.

(b) Ni kweli tunajua kwamba wanafunzi wetu wapo katika msongomano na tunajitahidi kadri inavyowezekana kama tulivyosema kwamba tutajenga skuli kama kumi katika kipindi kupunguza msongamano katika sehemu nyengine na niseme tu hata katika Jimbo la Mwakilishi pale Kijitoupele tutamjengea naye Skuli ya Msingi.

Nam. 12

Kuzalisha Chakula cha Kutosha Ndani ya Nchi

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali yetu ina mpango wa kuimarisha kilimo nchini ili kuzalisha chakula cha kutosha na kuachana na mpango wa kuagiza chakula kutoka nje. Na vikundi vingi vya kilimo na mifugo vinajitahidi kuzalisha mazao mbali mbali lakini bado vikundi hivyo havijawa na uwezo wa kuzalisha mazao ya kutosha ili kufikia azma ya Serikali ya kutoagiza chakula kutoka nje ya nchi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviendeleza na kuviongezea nguvu ya kifedha na utaalamu vikundi hivyo ili kuongeza uzalishaji zaidi na kuondoa tatizo la chakula katika nchi yetu.

(b) Je kuna vikundi vingapi vinavyotambuliwa ambavyo serikali imejipanga kuviendeleza kwa kusaidia uzalishaji wa chakula nchini na lini serikali itatimiza azma yake ya kuacha kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan wa Jimbo la Chake Chake swali lake nambari 12 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Wizara inaendelea na mpango wa kutoa taaluma kupitia kwa wakulima wa mazao ya chakula na ya kibiashara ili kuongeza uzalishaji wa chakula. Kupitia msaada kutoka benki ya dunia, Wizara inatekeleza mradi wa ERPP ambapo hekta 193.3 zitaendelezwa kwa kuwekewa miundo mbinu ya umwagiliaji maji.

Aidha, mradi utatekeleza kipengele cha mfumo endelevu wa uzalishaji mbegu sambamba na kutowa taaluma ya kilimo bora cha uzalishaji mpunga kwa kutumia mbinu za kilimo shadidi (SRI), ambapo hadi sasa wakulima 1,110 wameshapatiwa mafunzo ya kilimo shadidi, jambo ambalo litaongeza uzalishaji kutoka tani nne kwa hekta na kufikia tani nane kwa hekta, ambapo lengo la mradi kwa mwaka ni kuwapatia wakulima 1,110.

Mhe. Mwenyekiti, vipo vikundi 1500 (skuli za wakulima Unguja na Pemba) ambapo vimepatiwa taluma za kilimo cha kisasa ikiwemo ukulima wa migomba, muhogo na mboga mboga. Mhe. Mwenyekiti, mbali na juhudi hizo Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Taha kushirikiana na *Milele Foundation* imewapatia wakulima *solar pump* 10 kwa matumizi ya kilimo cha umwagiliaji maji. Pia vikundi 8, vitano Unguja na vitatu Pemba vya wakulima vimepatiwa mkopo wenye thamani ya shilingi milioni sabiini na moja kutoka katika mfuko wa uwezeshaji uliopo chini ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri nataka niongezee tu kidogo kwa swali (a) na (b). Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba katika vikundi ambavyo wamevisaidia sijui kuna kikundi

kilichojihusha na viwanda vya *juice* au ninaweza kusema ukamuaji wa juice au hakuna na kama vipo wamevisaidiaje. Na kama kusaidiaje kama havipo kabisa, Serikali inachukua hatua gani kwa sababu sasa hivi matunda kama maembe Pemba ndoo nzima ni shilingi elfu moja yanapotea vibaya sana na ikiwa yale ni matunda halisi. Je, kama havipo Serikali inachukua hatua gani katika kuwashajihisha watu hawa.

Swali langu la pili jana Waziri wa Afya alizungumza kwamba kuna matunda ambayo ameshazungumza na wataalam ambayo kwa Zanzibar yamepotea sasa imekuwa ni tatizo na ndio yanayotusababisha kupata maradhi mengi, ambavyo naweza kusema alisema sijui kama pilipili doria na kitu gani. Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha mimea hii katika enzi zake.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa masuala yake (a) na (b). Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Serikali ina mpango wa kutengeneza kituo cha *agro processing* kama tulivyosema ili tuweze kuhifadhi matunda yetu haya na kama tukiweza tuweze kufanya hata hizo *juice*. Mwisho jana Waziri wangu amekwenda Pemba kuangalia eneo hilo la kituo cha *agro processing* kwa Pemba.

(b) Matunda ni kweli yanapotea matunda yetu ya asili lakini ukija katika vituo vyetu vya *nursery* kama pale Maruhubi basi tunayo hiyo pilipili doria uliyosema, michongoma na miche mengine. Ahsante.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili na Mifugo swali langu lenye kifungu (a) na (b)

(a) Kuna hekta 199 ambazo wameziwekea miundo mbinu, miundo mbinu hiyo ni ya udongo au kwa kutumia matofali.

(b) Kuna vikundi ambavyo wamevisaidia, kawaida kwa wananchi sasa hivi aghalabu huwa wanavisaidia vikundi vya mjini tu, sasa nataka aniambie ni kikundi gani na kiko wapi ambacho kimepata msaada.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

(a) Mhe. Mwenyekiti, unapotengeneza miundo mbinu ya umwagiliaji maji ukitengeneza ya udongo maana yake haitokuwa madhubuti, miundo mbinu yetu ni ya saruji.

(b) Anasema ni vikundi vingapi kama sikosei, vikundi ambavyo tumevisaidia kwa Unguja na Pemba ama ni kwa Unguja peke yake. Kama ni kwa Unguja basi ni Mpapa, Bambi, Kiboje, Kombeni, na kwa Pemba ni Vitongoji, Kangagani, Weleni Tumbe na Konde.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nina maswali mawili madogo sana ya nyongeza. Kwa vijana wetu wameitikia wito baada elimu yenu mlioitoa na kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa matunda kuwa mengi kama maembe, matikiti na mananasi. Wizara unayoiongoza mtawatafutiaje soko hili baada ya kuwapa elimu na mazao yao kuoza na kushindwa kuyauza, matitikiti, mananasi na maembe imekuwa mkitoa elimu tu kuotesha vitu hivi lakini soko mtawatafutia lini.

La pili swali la msingi alilouliza Mhe. Suleiman, je, kuna vikundi vingapi vinavyotambuliwa ambavyo Serikali imejipanga kuviendeleza kwa kusaidia uzalishaji wa chakula nchini na lini serikali itatimiza azma yake ya kuacha kuagiza chakula. Swali langu la msingi

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa wewe huna swali la msingi wewe swali la nyongeza, uulize swali la nyongeza kutokea swali la msingi, endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nasema swali la msingi lililoulizwa na Mhe. Suleiman, sio swali langu mimi. Suala la kutaka kujua lini serikali itaachana kuagiza chakula pana *Hansard* ya tarehe 09.06.2016 naomba ninukuu.

"Mhe. Spika kwa hiyo tukizungumzia sekta ya mpunga tu peke yake katika kipindi cha miezi sita waheshimiwa nitawachukua mkatembee mkaone hali ilivyo na mimi nimemwambia Mhe. Rais Shein kama nilivyowahi kumwambia Rais Nyerere, nilimwambia miezi sita kama sijalisha magereza najiuzulu nimwambie Shein ikifika miaka mitatu kama hatujaagiza mchele hapa bora tu nikuwachie wizara yako"

Je, Mhe. Waziri nia hii anayo kweli ya kujiuzulu mwaka mmoja na nusu tayari ushafika bado mwaka mmoja na nusu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana mwenyekiti napenda kumjibu Mhe. Jaku masuala yake kama ifuatavyo:

Kwanza nimwambie kwa taarifaa tu tuna duka pale maruhubi la kilimo ambalo linaunganisha wafanyabiashara na wakulima wa aina mbali mbali walete mazao yao ili tuweze kuwapatia yale masoko, mpaka sasa duka liko karibuni waheshimiwa.

Swali lake namba (b) ni kweli Mhe. Waziri ameahidi hiyo ahadi tumuombe Mwenyezi Mungu utafiti wetu huu tunaoufanya sasa hivi kwa kilimo cha shadidi kupitia ambacho kinatumia maji kidogo na mbegu kidogo na mavuno mengi tumuombe Mwenyezi Mungu atukubalie mvua ziwe kwa wingi na vile vile hiki ni kilimo cha umwagiliaji ambacho hakitumii maji mengi basi mazao yatakuwa mengi na In Shaa Allah kwa muda wa miaka mitatu tutaacha hii kugiza michele kutoka nje ya nchi. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri karibu utoe majibu mazuri zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti nataka nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri na fasaha kabisa.

Niseme kwanza ni kweli kwamba wananchi nataka niwapongeze kwa dhati kabisa wameitikiwa wito wa uzalishaji baada ya kutoa taatuma tuliyoitoa na mazao yamekuwa mengi kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu katujaalia baraka hii kwamba sasa mazao yamekuwa mengi kuna haja ya kujenga viwanda.

Lakini nataka kumshukuru vile vile Naibu Waziri alipoelezea juu ya suala la duka ambalo tumelianzisha baada ya kuona kwamba mazao yamekuwa mengi na sasa Rais ametuagiza anataka aone mchele au mazao yanatokana na *brand* ya Zanzibar imekuwa kila siku tunanunua mchele wa Mbeya, tuna mapembe na kadhalika sasa wanataka tuone mchele kutoka Zanzibar.

Naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba hatua ya kwanza tumeanzisha hiyo *centre* ya kuweza kutoa, tumechukua mayai kutoka Pemba, tumechukua bidhaa mbali mbali sasa hivi tuna mafuta ya alizeti tunayo pale dukani, sukari inayozalishwa Mahonda tunayo pale tumeshatengeneza *packing* rasmi ya mchele wa Zanzibar, tunategemea baada ya miezi miwili itakuwa tayari. Kwa

hiyo, tunajitahidi sasa kwenda nayo haya masuali lakini nataka niseme jambo la kwanza ilikuwa suala la uzalishaji mimi nataka niwapongeze sana wakulima kuwa wameitikia suala zima la uzalishaji sasa tufundishe namna ya kuhifadhi mazao hii ndio kazi tunayoifanya sisi tumefikia na wizara yetu ya Maendeleo ya Vijana tunashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara namna gani ya kuweza kuhifadhi mazao.

Mbali tuko katika soko kwanza kuhifadhi yale mazao yenyewe hii ndio kazi tunayoifanya ndio maana tuna hizo *agro processing plant* iko moja Pujini jana nimekwenda kuikagua nimeambiwa baada ya miezi sita itakuwa tayari na nyengine iko Kizimbani tunagemea vile vile baada ya miezi sita nayo wenyewe itakuwa tayari. Kwa hivyo angalau tutakuwa usiwinde wa hifadhi wa mazao yasiharibike hiyo sehemu hiyo itakuwa imefanyika tunawafundisha watu namna ya *parking* ya mazao yenyewe na vile vile tunawafundisha mazao gani yanatakiwa kwa soko gani hizo hatua tumezichua tunaamini zitakamilika.

Suala la kujitosheleza kwa chakula sisi tumezoea kwamba mchele peke yake ndio chakula. Chakula maana yake ni mchele, muhugo, ndizi, viazi na kadhalika ikitimia ile *balance diet* ndio inatimia chakula kikamilifu. Nataka niwahakikishie wananchi kama tumepiga hatua ya kuweza kuzalisha mayai mpaka sasa hivi yanatafuta soko, kama tumepiga hatua ya kuzalisha maziwa hivi sasa, tunazalisha tani lita115,000 kwa siku sasa hivi. Hiyo ni hatua muhimu sana.

Sasa kumbe tuna uwezo wa kupata chakula cha kikamilifu cha binadamu wanaweza kula sio mchele peke yake, lakini hata hii ya mchele, mchele tunaagizia tani 80,000, sasa hivi hekta 1500 tunazomwagilia maji na hekta 1500 zitakazoingia katika mpango wa *Exim Bank* kwa uzalishaji wa kutumia shadidi tunaamini kabisa asilimia 60 - 70 ya mazao tulokusudia yapo. Na ahadi niliyoitoa bado narudia tena ahadi ile ipo na sitobadilika mpaka tuhakikishe kabisa nchi yetu inategemewa kwa chakula, cha msingi ni kujitegemea kwa chakula, hilo lazima lijulikane. Msingi kujitegemea nini, kwa chakula! Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa muda wa maswali umemaliza lakini tutaendelea, naomba tuendelee na swali lililobakia kwa sababu waziri anayefuata bado ana taarifa atatoa baadae lakini tumalizie swali letu lililobaki hili. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Mwenyekiti: Soma utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana kwa muongozo wa kiti chako. Nilichozungumza hapa mimi suala la matikiti, maembe na mananasi.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo kanuni hujaisoma ya utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 37

Mhe. Mwenyekiti: Isome

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. "Waziri, Mjumbe yeyote anayeuliza swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, swali analoulizwa anatakiwa kujibu kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi isipokuwa kwamba maswali aloulizwa waziri mmoja yanaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Mwenyekiti: Naam, sasa waziri ameshajibu hujatoshekeleza?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante. Mimi sikutaka mayai, nilouliza wananchi wetu wameitikia wito wa kiasi kikubwa wa matikiti sasa hivi njia ya Amani ukienda hata jioni yanabaki pale pale hawawezi kuchukua watu, haya soko Alhamdullillah Rabil-alamina maembe sasa hivi hata hayasemeki, mananasi yakifika wakati Donge jioni yanaachwa pale pale hayachukuliwi. Serikali imejipangaje kuwatafutia soko, swali hili, ndio nilouliza. Tusiwe na huruma kwa mdomo tu kwa vitendo tunawafanya nini wananchi wetu, washaitikia wito lakini bado serikali haijataka kuwatafutia soko, ndio swali langu liko hapo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, chombo chetu tunaendesha kwa mujibu wa kanuni, nashukuru Mhe. Mjumbe ame-*quote* kanuni, lakini kanuni alokoti hakumalizia. Kanuni ya 37 kwenye fasili ya 2 inakutaka wewe uliyekalia kiti cha Spika ndio utaye *determine* kama majibu yalikuwa sahihi au si sahihi na sio mjumbe. Kwa hiyo imani yangu wewe kuridhia kwako kunyamaza kimya maana yake majibu yalikuwa sahihi na hakuna sababu ya kupoteza muda tuendelee na shughuli zetu *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa kitako kwanza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Issa Gavu Waziri wa Nchi kwa kufafanua kanuni na vizuri tukaziheshimu hizi kanuni tukazitumia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kama mjumbe alinisikiliza vizuri na alimsikiliza Naibu Waziri alipokuwa anajibu alisema, katika suala la masoko tumeanzisha hata duka maalum ili watu bidhaa zao zije na wale wanaotaka kununua kwa *whole sale* waje wajue bidhaa zinapatikana wapi; hiyo ni *process* ya kujua soko liko wapi. Hilo la kwanza.

Lakini ili soko lifikie soko lazima lifikiwe na bidhaa ambayo inatakiwa ndani ya soko, ndio maana tumeanzisha *agro processing plant* mbili moja iko Kizimbani na moja iko Pujini ili tuwafundishe wakulima wetu baada ya kuzalisha je, soko linahitaji nini? Tunawafundisha namna ya *packing* na kadhalika, huu ndio utaratibu wa masoko sio kitu unachokizalisha unapata soko. Soko lina *demand* zake lazima uzi *meet* zile *demand* zinazotakiwa ndio maana tunachukuwa *process*.

Process ya kwanza ni kuzalisha, *process* ya pili ni kuhakikisha je, tulichokizalisha kinatakiwa sokoni ni kazi ya serikali kutoa taaluma hiyo ndio kazi tunayoifanya wananchi wajue soko linahitaji nini na nini. Kwa mfano, unaweza ukenda wewe ukakuta nanasi nataka kukupa mfano hai, mimi nilikuwa nazalisha mananasi.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nasafirisha kupeleka Oman, Dubai wakanambia nanasi unaloleta ni la kilo tatu huku tunanitaji nanasi la nusu kilo. Kwa hiyo mananasi ninayo lakini *demand* ya soko ni nusu kilo au robo kilo hasa hayo lazima uyajue kwa *process* ya kwanza kujifundisha mtu kuelewa kuzalisha. Umeshazalisha sasa twambie soko letu lina *demand* kwa *product* yako hii na kazi tunayoifanya ndio wajibu wa serikali kufanya kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wananchi wamekusikia nadhani ushauri wako wataufuata, katibu tunaendelea.

Nam 58

Ukosefu wa Watendaji wa Afya Ziwani

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:

Tatizo la Madaktari na Maodali katika Jimbo la Ziwani limekuwa kubwa na kupelekea wananchi wanaokwenda kutafuta matibabu katika vituo hivyo kukosa huduma wakati vijana wenye sifa hizo wapo.

Je, ni lini Serikali itawaajiri vijana hao ili waweze kutoa huduma kwa jamii ya watu wa Ziwani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kumjibu Mheshimiwa Suleiman Makame Ali Mwakilishi Jimbo la Ziwani swali lake Nam. 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe Mwakilishi kwamba kuna uhaba wa wafanyakazi kwa baadhi ya vituo vya afya na hili sio kwa vituo vya Jimbo la Ziwani tu bali ni kwa majimbo mengine Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na kwa ukaribu zaidi tayari imeshatoa ruhusa ya kuajiri madaktari yaani *Medical Doctor* na wafamasia wenye shahada ya chuo kikuu. Aidha serikali imetoa ruhusa ya kuajiri mafundi sanifu wa dawa *pharmacy technician* waliohitimu mwaka 2014 na wale waliohitimu mwaka 2015 katika chuo chetu cha Afya Mbweni.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo serikali pia imeshatoa ruhusa ya kuajiri wafanyakazi 221 wa kada ya afya ambao watakidhi viwango kwa mujibu wa Sheria za Utumishi, hivi sasa wizara yangu tayari inakamilisha ajira ya madaktari 44 na wafamasia 4 na wanaendelea kufanya hivyo kwa utaratibu maalum. Ahsante.*(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza nitakuwa mtomvu wa adabu wa mwisho kama sikushukuru kwa umakini wako jinsi unavyokiendesha kiti, nakupongeza sana na nimuombe tu Mhe. Naibu Waziri katika majibu ya swali la msingi alilouliza Mhe. Suleiman naomba ninukuu:

Tatizo la madaktari na ma-*orderly* katika vituo vya afya Jimbo la Ziwani limekuwa kubwa kwa wananchi lakini nimwambie tu vituo vingi vimekuwa na matatizo kama alivyokiri Mhe. Naibu Waziri nikushukuru kwa kukiri hilo. Lakini kuna vyengine hivi vituo havitaki hata ma-*orderly*, kama kitu cha Kitope hivi sasa kina ukosefu wa maji wananchi wanaambiwa wachukuwe maji yao ya kwenda kujisaidia vyooni kwenye vituo hili halitaki ajira mpaka liajiriwe kitu muhimu kweli kweli kituo cha Kitope kina ukosefu wa maji wacha hao ma-*orderly* na wafanyakazi wengine. Linataka jawabu lini haya maji yatapatikana wananchi wanazidi kuumia kule,

Lakini la pili umesema kuna wanyakazi 221 kada ya afya 44 madaktari, 4 wafamasia haya ni majibu ya Serikali siku zote niendelee kumshukuru Dr. Ali Mohammed Shein tena kwa umakini wake wa hali ya juu katika sekta ya afya kazi wanayofanya ni kubwa mno na sisi sote ni mashahidi humu lakini utendaji wenu bado hamjajipanga katika sekta ya afya. Naiuliza Serikali lini wataajiriwa hawa tusiwe kutamka kwa mdomo tu, lini wataajiriwa hawa ili wananchi wapate kuridhika nataka *commitment* ya serikali. Serikali inafanya kazi kwa pamoja Mhe. Issa Gavu hunyanyuka mara nyingi akajibu kuisaidia serikali naomba naye ainuke kutupa kauli hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti naomba kwanza nimjibu Mwakilishi wa Jimbo la Paje kwa niaba ya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani kwamba naanza kukujibu swali (b). Hii leo nilipoondoka ofisini asubuhi saa 3 kasorobo nimeacha watarajiwa waajiriwa hao 44 wanaingia taratibu kwa kufuata utaratibu ili kukamilisha *process* zao. *(Makofi)*

Kwa hiyo nategemea kwamba aidha leo wanaweza kukamilisha mipango yote kwa ajili ya uajari na kupangwa katika vituo mbali mbali mheshimiwa nakuomba uwe na subira na serikali iko mbioni kukamilisha tatizo hili kwasababu inajua tatizo kubwa linalowakabili wananchi.

Mhe. Mwenyekiti sasa naomba nimjibu swali lake namba (a) kuhusu suala la ukosefu wa maji kituo cha Kitope. Suala hili tunalo nakumbuka tulitoa agizo Kamati ya Afya pale ikae kwa sababu utaratibu wetu baadhi ya mambo madogo madogo huwa yanamalizwa na Kamati za Afya za ndani ya vituo, sasa sijapata *feedback* ya Kamati ya Afya iliyokaa pale na kujadili na kukubaliana nini wafanye, lakini naamini wakituletea mrejesho lile ambalo litawashinda mara nyingi wizara huwa tuna libeba na lina pata suluhisho.

Mheshimiwa naomba hili tulifuatilie pamoja kama ikiwa bado hawajakaa naomba wahimize wakae kwa sababu nafikiri hata wewe ni mjumbe katika

kamati hiyo ili walijadili tuone kwamba litawashinda basi tuanze kuangalia utaratibu mwengine tuhakikishe kituo kile kinapata maji. Maji ni muhimu hasa katika kituo cha afya.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuuliza na mimi swali la nyongeza katika Wizara hii ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi napenda kumuuliza swali la nyongeza. Katika jengo la Beit el Ras ambacho ni Chuo cha SUZA sasa hivi kuna kituo cha afya ambacho kituo hicho kina daktari mmoja tu na mule kuna wanafunzi ambao wanaoingia vipindi viwili asubuhi, mchana na jioni na kuna wanafunzi wengi na kituo hicho hutumika kwa walimu wanaoishi pale katika nyumba ile pamoja na wananchi ambao wanaoishi eneo lile. Lakini cha kushaangaza daktari ni mmoja tu na kituo kile inapofika saa tisa au sita daktari yule anaondoka kutokana na kazi nyingi alizokuwa nazo kwa sababu wanakuwa wanahitajika kutumika kwa kazi zote za kufunga vidonda na nyengine.

Je, serikali ina mpango gani wa kuongeza daktari katika kituo kile cha afya kwa sababu kituo kile sasa hivi inapelekea kujazana wagonjwa wengi katika kituo au hospitali ya Kibweni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti nakumbuka katika jibu kwamba tayari Serikali imeshatoa ruhusa ya kuajiri na katika ambao wafanyakazi wataajiriwa na madaktari wataajiriwa na kwa bahati nzuri Mhe. Rais katupa ruhusa ya kuajiri madaktari wakati wowote bila ya kuomba hata ruhusa. Kwa hiyo, nakukuhakikishia mheshimiwa *process* hii itakapokamilika na tukaajiri basi hakikisha kwamba katika madaktri ambao tutawasambaza na katika kituo hicho tutahakikisha tunapeleka madaktari wa kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya moja la nyongeza kama ifuatavyo, pamoja majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba nimuulize suala moja kwa kuwa vituo vingi vya afya vina ukosefu wa wafanyakazi ukizingatia kwamba kituo changu cha afya kilichopo katika Shehia ya Junguni kimefunguliwa juzi tu na Mheshimiwa Waziri Juma Ali Khatibu *(Makofi)*

Kituo hicho ni kwa ajili ya kinamama kujifungulia pale pale kuondokana na usumbufu wa kwenda Wete na ukizingatia kwamba madaktari waliopo katika kituo kile cha Junguni ni watatu hutibu homa ni wao, wajawazito ni wao na kila kitu ni wao. Je, wizara ina mpango gani wa kuwachukua wafanyazi waliopo

katika shehia ile ile ya Junguni kuondokana na usumbufu wa kina mama wanapojifungua na je, ni lini kituo hiki kitaanza kufanya kazi,

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsasnte Mhe. Mwenyekiti mimi napenda nimjibu suala lake la nyongeza Mhe. Maryam mwakilishi wa jimbo la Gando kama ifuatavyo.

Kwanza naomba nirekebishe kidogo kituo hichi hakijafunguliwa na Mhe. Juma isipokuwa kiliwekwa jiwe la msingi kitakachofuata wakati wowote kuanzia mwezi wa Machi kinaweza kikafunguliwa.

Mhe. Maryam nakuhakikishia kwamba kupitia ajira hizi kituo cha afya cha Junguni kitapata wafanyakazi wa kuweza kutoa huduma ya uzazi pamoja na huduma nyengine. Kuhusu suala la kuwapata wafanyakazi wa kijiji kile cha Junguni au cha Gando cha maeneo ya karibu suala hilo Mheshimiwa naomba utusaidie kwenda kuwasomesha vijana ambao wako katika jimbo lako ili wakati ukifika basi wawe tayari kuajiriwa katika kituo kilicho karibu na jimbo lao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tumemaliza muda wa maswali, ya nyongeza pia tayari tumemaliza.

Waheshimiwa wajumbe kama nilivyosema awali suala letu hili litakuwa la mwisho sasa kwa sababu katika *order paper* yetu ya leo ilionesha hoja ya serikali hapa lakini waziri husika kuna mambo fulani hajaweka vizuri. Kwa hivyo, tutengue kanuni ya muda ili kwa leo tuahirishe mpaka saa 11 jioni. kwa hivyo Mheshimiwa Waziri Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais karibu sana tupe taarifa.

KUAHIRISHA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini Mhe. Mwenyekiti kabla ya kuliomba Baraza lako tukufu kutengua kanuni ya muda ningeomba nitoe maelezo mafupi yafuatayo.

Kutokana na yaliyojitokeza katika baadhi ya vyombo vya habari kuhusu mswada wetu wa sheria ya kufuta sheria ya Tume ya Uchaguzi namba 9 ya mwaka 1992 na kutunga sheria ya kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar majukumu yake, uwezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa kuna baadhi ya vyombo vya habari vimetafsiri vibaya kuhusu maamuzi ya Tume, kuna wanaotafsiri kwamba sheria hii imetoa uwezo maalum kwa Mwenyekiti wa Tume kufanya maamuzi ya Tume bila ya kushirikiana na Tume yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti maamuzi ya tume yanatokana na kifungu cha katiba cha 119 (10) ndio kinachoipa uwezo wa kufanya maamuzi, na sio Mwenyekiti kwa maana Mwenyekiti binafsi. Mwenyekiti ni sehemu ya Tume kwa hiyo kuna utaratibu wa kikatiba unaotoa muongozo kwa namna gani Mwenyekiti anatangaza hayo maamuzi ya tume. Kwa hiyo si sahihi kusema kwamba sheria hii imempa uwezo Mwenyekiti wa Tume, tulieleza vizuri Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe sababu za kuanzishwa sheria hii.

Kwamba moja ilikuwa kuna mgongano wa sheria ilivyo na katiba ya Zanzibar ndio maana tukafanya marekebisho hayo, na jengine ilikuwa ni kuipa uwezo Tume yenyewe kuanzishwa kwa Ofisi ya Tume ya Uchanguzi pamoja na vitengo vyake, na nyengine kuanzishwa ofisi za uchaguzi za wilaya pamoja na uundwaji wa kamati za ushauri kwa masuala ya uchaguzi.

Hayo ndio yalokuwa mambo ya msingi yaliyosababisha kufanywa mabadiliko ya sheria pamoja na kuipa tume uwezo wa kutumia majengo ya serikali na binafsi kwa shughuli za uchaguzi na kuainisha makosa na adhabu. Hakuna mahala popote katika kikao hiki ama katika sheria hii iliyompa mamlaka Mwenyekiti peke yake ya kufanya maamuzi kwa niaba ya Tume.

Kwa hiyo, ningependa vyombo vya habari na wananachi na watu wote wanaotusikiliza waelewe dhamira njema ya serikali kwamba katika sheria iliyokuwepo kulikuwa na mgongano kati ya sheria na matakwa ya katiba ndio maana tumefanya hivyo, kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba na kisheria ili asitokee mtu kupotosha ukweli huo. Dhamira yetu ilikuwa njema, dhamira yetu safi, nia yetu ni kuiboresha sheria hii iweze kufanya kazi vizuri zaidi kwa matakwa ya katiba.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Mwenyekiti sasa niliombe Baraza lako tukufu kwa kuwa Waziri na watendaji wake baada ya maelezo mazuri ya na msingi yaliyotolewa ufafanuzi katika sheria yetu hii iliyo mbele yetu kama inavyoeleza *order pape*r ya leo na kwa sababu kuheshimu maelezo hayo ya waheshimiwa wajumbe tungeomba muda zaidi wa kujitayarisha ili tuwe na majibu mazuri katika hoja hii ya mswada wa sheria ya kufuta sheria ya nembo namba 1 ya mwaka 1985 na sheria ya Bendera ya Zanzibar namba 12 ya 2004 na kutunga sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya

Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa kwa Zanzibar ya mwaka 2016 na mambo mengine yanayohusina na hayo ili tuweze kuifanya kazi hii ya majumuisho vizuri jioni hii.

Kwa hiyo, naliomba Baraza lako tukufu tuweke kando kanuni ya muda ili sasa hivi tusitishe shughuli zetu mpaka jioni ya leo saa 11:00 barabara tuweze kuendelea tena na kuja kufanya majumuisho ili kwa pamoja tuweze kupitisha sheria yetu hii muhimu kwa maslahi yetu na wananchi wake.

Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa mmeyasikia ya Mheshimiwa kwa hivyo naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo nami niwashukuruni kwa utulivu wenu na mawaziri kujibu maswali na waheshimiwa kuwa makini katika majibu yetu tuliopewa. Kwa sasa naliahirisha Baraza hili hadi hapo saa 11:00 jioni kwa kuendelea kwa mswada ulio mbele yetu.

Ahsanteni

(Saa 4.45 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili tuweze kufanya majumuisho na Mwenyezi Mungu akitujaalia tuweze kuwa na sheria yetu ambayo iliyobora inayohusiana na masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba uniruhusu niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mara nyengine juu ya umakini wao na umahiri wao katika kujenga hoja mbali mbali ili kutupa mashauri ambayo siku zote yanatuelekeza

katika kufikia maamuzi ya busara. Aidha, nichukue fursa hii kuishukuru sana kamati kwa mapendekezo yake ya msingi ambayo imeeleza mambo kwa upana na sisi tunakubaliana sana na maoni ambayo kamati wameyatoa. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru sana watendaji katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba sheria yetu hii inafikia ukingoni vizuri na kwa salama.

Mhe. Naibu Spika, hoja hii imechangiwa na wajumbe 30, kwa upande wa wajumbe waliochangia kwa maneno walikuwa ni 14, na waliochangia kwa maandishi walikuwa ni 16. Kwa hivyo, kwa ruhusa yako mheshimiwa naomba uniruhusu niwatambue wajumbe. Kwa wale ambao waliochangia kwa maneno ndani ya Baraza lako tukufu nianze na Mhe. Simai ambaye yeye licha ya kuchangia mwenyewe binafsi lakini pia aliwasilisha hoja ya kamati.

1. Mhe. Simai Mohammed Said
2. Mhe. Shehe Hamad Mattar
3. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
4. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
5. Mhe. Ali Khamis Bakar
6. Mhe. Suleiman Sarahan Said - jembe lisilo mpini
7. Mhe. Panya Ali Abdalla
8. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
9. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
10. Mhe. Omar Seif Abeid
11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Khadija Omar Kibano
13. Mhe. Rashid Makame Shamsi
14. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Kwa upande waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Rashid Ali Juma
2. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Bahati Khamis Kombo
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma
6. Mhe. Shamata Shaame Khamis
7. Mhe. Nassor Salim Ali
8. Mhe. Asha Abdalla Mussa
9. Mhe. Hamida Abdallah Issa

10. Mhe. Said Omar Said
11. Mhe. Ussi Yahya Haji
12. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
13. Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
14. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
15. Mhe. Miraji Khamis Mussa
16. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla wake waheshimiwa hawa maoni yao waliyoyatoa sisi tunaona ni mawazo ya busara, lakini mawazo mengi yalikuwa ya ushauri. Kwa hiyo, kwa njia moja au nyengine tunaupokea ushauri wao.

Mhe. Naibu Spika, michango mingi ilielekezwa katika kifungu Nam. 7 cha sheria ambayo sana kilikuwa kimeelekeza kwenye suala la kupiga marufuku matumizi ya bendera. Lakini vile vile na kifungu Nam. 8 kuhusu uwezo wa waziri wa kutunga kanuni na kifungu Nam. 9 kuhusu waziri kusamehe.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kueleza hayo moja baada ya moja ningeomba nitoe maelezo mafupi ya jumla kama utangulizi wa maelezo yangu.

Mhe. Naibu Spika, nianze kusema kwamba chombo chetu hiki cha Baraza la Wawakilishi ni chombo kikubwa sana, na sisi Waheshimiwa Wajumbe tuliokuwepo hapa tunawawakilisha wananchi wetu kutoka majimboni kwetu tunakotoka. Kwa hivyo, michango yetu yote lazima ielekeze katika suala zima la kuimarisha umoja wetu, upendo wetu na dhamira ya kuhakikisha kwamba tunafanya mambo bila ya kuonesha ishara ya aina yoyote kwa njia moja au nyengine kuona mtu yeyote yule kumbagua mwengine. Kwa hiyo, ni vizuri sana kwenye michango yetu tukaelewa kwamba Zanzibar ni nchi yetu na sote tunapaswa kufanya kazi kwa pamoja kujenga nchi hii, ilimradi tunatekeleza misingi ya Katiba na sheria ili siku zote tuendelee kuwa wamoja na kujenga nchi yetu ipige hatua kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kulikuwa na kauli ambayo kwa njia moja au nyengine katika suala zima la wimbo wetu ule wa Taifa, tulikuwa tumependekezwa kwamba badala ya neno “Jamhuri” tuweke neno “Mapinduzi”.

Mhe. Naibu Spika, dhamira ya Mapinduzi yetu ilikuwa ni kuleta Jamhuri, msingi wa Jamhuri ni kwa wananchi wenyewe kuamua mambo yao katika nchi yao, na kwamba wananchi wote ndio wawe na mamlaka katika nchi yao kusiwe na mtu au kikundi cha watu au ukoo wa watu ndio ambao wana mamlaka juu

ya nchi yetu. Kwa msingi huu neno “Jamhuri” ni kwa ajili yetu sote. Kwa hiyo, ndio maana katika wimbo wetu ule kwa kuonesha kielelezo cha Mapinduzi matukufu kwamba dhamira yake yalikuwa ni kuleta Jamhuri, kuleta usawa, kuleta maridhiano, kuleta umoja katika nchi yetu ndio maana katika wimbo ule kukawa na neno la “Jamhuri”. Kwa msingi huo bado sisi tunaona neno “Jamhuri” libakie katika wimbo huu, na ukitazama ni neno ambalo ni letu sote, linaleta haiba na hadhi kwetu sote kwa sababu Mapinduzi ni kitendo kilicholeta Jamhuri. Kwa hivyo, bado tukiweka Jamhuri tunaendelea kuheshimu Mapinduzi yetu na Mapinduzi yetu yanakuwa tunaenda nayo sambamba.

Kwa nini tunauwita wimbo wa Taifa? Nyimbo nyingi za kitaifa duniani kama hizi zinaitwa *National Anthem*, hatuna tafsiri nyengine ya Kiswahili zaidi ya kusema ni wimbo wa Taifa, maana huwezi kuuwita wimbo wa nchi lakini kwa tafsiri sahihi ya Kiswahili ndio maana tunauwita wimbo wetu wa Taifa, kwa sababu ya hadhi yake, kwa sababu ya heshima yake na kwa sababu ya umuhimu katika nchi yetu. Kwa hivyo, naamini Mhe. Mjumbe utakubaliana na mimi kwamba tunaposema wimbo huu ni wimbo wetu wa Taifa utakuwa unamaana kwa msingi huo, kwa sababu hakuna lugha nyengine ya Kiswahili tutaitafsiri *National Anthem* kwa namna yoyote zaidi ya kusema wimbo wa Taifa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la umuhimu wa elimu kwa umma, nataka nikubaliane na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ambaye alilizungumzia sana jambo hili. Ni kweli upo umuhimu sana ya kutoa elimu kwa umma ili wananchi waelewe vielelezo vyetu vya kitaifa ikiwemo nyimbo ya Taifa, ikiwemo nyimbo ya ukombozi, ikiwemo nembo yetu, bendera yetu na maana ya rangi zile za bendera kwa hiyo ni jambo la msingi sana kwa mambo haya kuelimishwa katika umma. Lakini pia naupokea ushauri wake wa kusema upo umuhimu wa kuheshimu na kuipa heshima maalum nyimbo yetu ya Taifa, nembo yetu na bendera yetu na ndio maana tunatunga sheria hii kwa msingi mkuu wa kuipa heshima maalum na hadhi yake. Naamini itakuwa kwa kufanya hivyo tumeweka heshima na hadhi ya nyimbo yetu ya Taifa pamoja na nembo yetu.

Mhe. Naibu Spika, eneo kubwa ambalo waheshimiwa walilizungumza sana ni hiki kifungu cha 7 chenye kuelezea kuhusu kupiga marufuku kutumia bendera, nembo ya serikali na wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo.

Kama alama ya biashara au kuambatanisha juu ya bidhaa yote au kuambatanisha juu ya bidhaa yote ya kuuza au kuzalisha au katika kuboresha matangazo na matangazo kwa ajili ya biashara yote ya viwanda, wito au

taaluma au kama ni nembo ya chama cha siasa au kama pambo au mambo ya sanaa au kuchapishwa zaidi kwa nembo au picha au kwa namna yoyote ile iliyokatazwa na sheria hii. Baada ya kutafakari kwa kina maelezo ambayo wajumbe wameyatoa na baada ya kutafuta mifano ya nchi mbali mbali tumeona upo umuhimu wa kugawa sehemu badala ya kuchanganya pamoja bendera, nembo na nyimbo sasa tuweke kwa sehemu bendera iwe na sehemu yake, nembo iwe na sehemu yake, nyimbo ya Taifa na ile nyimbo ya ukombozi iwe na sehemu yake.

Lakini baada ya kushauriana na wenzetu wanasheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na mifano mengine, bado tumeona upo umuhimu wa kupiga marufuku baadhi ya maeneo kama ambavyo mtaona jadweli litakalogawiwa kwa sababu inawezekana kabisa kabisa na kwa sababu ya mifano na nchi nyengine duniani kama vile Singapore, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata Kenya tumetizama sana wenzetu na tumeona kwamba mfumo wetu na mfumo wao unalingana sana. Kwa msingi ule ule wa kuipa heshima bendera yetu, kuipa hadhi bendera yetu na matumizi yake, lakini bado itakuwepo nafasi kwenye kanuni kwa ajili yale matumizi ya uzalendo pale ambapo inapotokea kuhitajika kutumika kwa wananchi wenyewe. Kwa mfano, inapotokea timu yetu ya mpira inataka kwenda katika mashindano ya kimataifa au shughuli nyengine basi pale inakabidhiwa rasmi na shughuli hiyo itafanyika. Halikadhalika katika matumizi mengine ambayo tutayaona kinchi tunataka yatumike hatutokuwa na tatizo kuitumia kwa sababu naamini kabisa kwamba watu wetu wanapenda waipe heshima yake, waipe hadhi yake na ionekane ni kielelezo thabiti cha wananchi wa Zanzibar. Na ni muhimu sana kutumia bendera yetu kuendeleza uzalendo wake.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ukubwa wa bendera kuwekewa kiwango kimoja. Mifano ya bendera mliopewa waheshimiwa umeonesha uhusiano wa pana, urefu na sehemu zilizo ndani ya bendera kwa maana ya *ratio* haikuelezwa kama ni *centimeter*, nchi, futi na kadhalika. Lengo la namba hizo ni kuwa kipimo chochote utakachochukua uzidishe kwa namba hizo ili umbo na uwiano wake usibadilike kwa bendera, ikiwa ipo kubwa au hadi ile ndogo kabisa. Kwa hiyo, msingi wetu zitakuwepo bendera za *size* kubwa, za *size* ya kati, za *size* ya ndogo ndogo kulinganisha na haja na matumizi na ufafanuzi zaidi utatolewa ndani ya kanuni. Kwa hivyo, ningependa kusema kwamba wale walioshauri kuwa na kitambaa pia kiwe ni kitambaa rasmi, nakubaliana nao kwa asilimia mia moja. Bendera yetu lazima iwe na hadhi, yenye kitambaa chenye hadhi, yenye rangi zinazokubalika zenye hadhi na kadhalika. Kwa hivyo, yote haya ya msingi mliotuambia tunaunga mkono na tutayafanya kama ambavyo mmetuelekeza. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu uchapishaji wa bendera. Uchapishaji na usambazaji wa bendera kwa matumizi ya serikali na taasisi zake unafanywa na serikali chini ya wizara inayosimamia Bohari Kuu ya Serikali na inapochapisha itazingatia rangi ambazo zimewekwa kisheria. Pia nachukua fursa hii kujibu swali liloulizwa kuwa ufito wa rangi nyeupe unamanisha nini? Jibu lake ni kwamba unamaanisha amani ya nchi yetu. Rangi nyengine zimeelezwa vizuri ndani ya jadweli naamini nyote mtaridhika maelezo yale ambayo yamo ndani ya jadweli.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu muda wa kupeperusha bendera. Muda wa kupeperusha bendera ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni na watu wanapaswa kuheshimu upandishaji wa bendera na ushushaji wa bendera na kanuni zitaeleza utaratibu wa kupandisha na kushusha bendera ya serikali.

Kuhusu waziri kusamehe, hapa kulikuwa na tafsiri kama kwamba waziri anasamehe kwenye hukumu. Sio, si suala la waziri kusamehe kwenye hukumu. Hapa bora hata lugha tukaiboresha kwa kusema kuondoa au kupunguza masharti. Kwa mfano, kuna mambo ambayo yameshurutisha kuhusu bendera, lakini kunapotokea jambo muhimu linataka lifanyike kuhusu bendera ndio hapo sasa waziri ataondoa sharti ile kama tunavyofanya katika kutengua kanuni, si msingi kwamba tayari umepewa adhabu waziri atafuta adhabu, hana uwezo huo. Lakini ni mambo ambayo yatatokezea ya matumizi ya bendera yetu, ama ya nembo yetu na kadhalika basi inapotokea uhitaji wa kufanya hivyo iwe kuna nafasi kwa waziri kuondoa hilo sharti ili matumizi yawe mazuri, yawe ya hadhi, yawe ya heshima yake.

Kuhusu matumizi ya nembo ya serikali katika biashara au alama za biashara. Kuhusu matumizi ya nembo ni kama tulivyokwishaeleza katika mswada, kwamba kwa ajili ya serikali mambo yanayohusiana na serikali si vyema kutumika katika biashara au kuwa sehemu ya shughuli za biashara, ile Nembo ya Serikali itatumika kwa shughuli za kiserikali. Kwa hiyo, haitotumika kabisa kwa shughuli za biashara za binafsi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maana ya vitu vilivyomo katika Nembo ya Serikali kumeulizwa maana ya mapanga na shoka. Naamini sote tunaelewa kwamba panga na shoka kwanza ni silaha yetu ya jadi, ni jambo la kushangaza sana kwamba mpaka leo tunauliza nini maana ya panga na shoka kwa matumizi ya Zanzibar. Haya ni matumizi yetu ya jadi tumeyatumia kwa maisha yetu kwa kutengezea shughuli zetu za kiuchumi na kilimo. Ukitizama kwa undani zaidi hata ukombozi wetu unatokana na panga na shoka. Kwa hiyo, jambo kama hili

Mhe. Mwakilishi anauliza maana ya panga na shoka katika nchi yetu kidogo haileti ile sura ya kuelewa undani na umadhubuti wa namna gani ya uzalendo wetu. *(Makofi)*

Kuhusu kutunga kanuni, kuna wajumbe wengine walitaka kanuni nazo zitungwe kwa haraka. Tunakubaliana nalo baada ya kupitisha sheria na baada ya kutiwa saini na Rais utaratibu wa kutunga kanuni utafuata mkondo wake. Lakini nataka niseme tu, tumesema sana suala la kutunga kanuni kwa waziri na wengi hapa walishauri kuwa kanuni zikitungwa zikapitishwe Baraza la Mapinduzi. Kwa sababu sheria hii iliweka kanuni mbili zile kubwa zaidi ndio zikapitishwe Baraza la Mapinduzi, lakini wengine walishauri ikapitishwe Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa niwajuilishe kuwa kimsingi na kimtazamo utafikiri waziri ndiye anayetunga kanuni, ni kweli waziri anatunga kanuni lakini kanuni zina mchakato mrefu zinaanzia wizara husika kwa wanasheria wa wizara husika kukaa hapo, lakini chanzo chake ni sheria yenyewe ndio inayoelekeza kanuni ziweje. Baada ya hapo inakwenda Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zinatizamwa zikoje, zinaendana na sheria au kuna kasoro zozote, na baadae sasa kwa mujibu wa kanuni yetu ya Baraza la Wawakilishi kuna kamati ndogo ya kushughulikia kanuni na sheria ndogo ndogo. Kwa hivyo, msingi ni nini, kitakachotungwa chochote kitakuja tena kwenye Baraza la Wawakilishi, hivyo haitokei kwa waziri kutunga kanuni kwa maslahi yake ni kinyume cha utaratibu kabisa, lazima kanuni zitatungwa kwa mujibu wa sheria yenyewe ili ziendane na matakwa ya sheria na ndio baadae zina mkondo wa kupitia mpaka kufikia kanuni hizo zitumike. Sidhani kwa utaratibu wetu katika nchi yetu kwamba mtu aliyepata sifa za uongozi akapata fursa ya kuchaguliwa mpaka kufikia *level* ya waziri akawa bado hajui utaratibu ajifanyie mambo yake na mama watoto nyumbani aje alete hapa na zikubalike, hilo jambo litakuwa haliwezekani.

Kwa hiyo, uamuzi ni wao Waheshimiwa Wajumbe wakiona kuna ulazima ziende zote Baraza la Mapinduzi kwetu ni sawa, wakiona zile mbili kubwa ambazo tayari serikali imeona zipelekwe Baraza la Mapinduzi na zilizobaki waziri awe na uwezo wa kuzimalizia kwa kufuata mchakato niliousema sawa, sisi tunachokitaka hapa ni kufanya mambo ambayo yataleta maslahi kwa nchi yetu na manufaa kwa watu wetu wote.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu udogo wa adhabu za makosa mbali mbali. Wajumbe wengi walitaka adhabu ziongezwe lakini sisi bado tunaomba na kuwanasihi wajumbe kwamba adhabu zilizomo kwa sasa tunaamini zinakidhi haja kwa

mujibu wa hali halisi ilivyo na mazingira yaliyopo, kama kutatokea watu kuitumia visivyo fursa hii au sheria hii wakaona adhabu hii kwao sio adhabu sahihi basi Mwenyezi Mungu akitupa uhai kama kuna mambo ya namna hiyo tunaweza kuja kufanya mabadiliko ya kuongeza adhabu. Lakini kwa uzoefu wangu tokea kabla hata hii sheria iliyokuwepo mwanzo sijaona kutokea tatizo kubwa. Kwa sababu watu wetu wameelimika kiasi cha kutosha ya kuheshimu vielelezo vya nchi yetu na adhabu hii ambayo imetolewa kama wapo watu ambao hata adhabu hii wataiona ndogo basi kuja hapa tukaleta marekebisho ya sheria tukawa na adhabu iliyo kubwa zaidi ni uamuzi wetu kwa pamoja. Lakini sisi baada ya kushauriana na wataalamu wetu na kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tunaona kwamba adhabu hii ya faini iliyomo na kifungo kilichomo inakidhi haja kwa atakaefanya makosa.

Kuhusu wimbo wa taifa na wimbo wa mashujaa kuimbwa katika skuli zetu zote za serikali na za binafsi ushauri huu kwetu sisi tunaona ni ushauri wa msingi na ushauri wa maana sana. Kwa hiyo, kwenye utaratibu wa kanuni tunaweza kuweka lakini hata kwenye utaratibu wa kawaida tu wa kiutawala unaweza kutoka utaratibu ili nyimbo hizi muhimu za taifa letu, nyimbo zetu za ukombozi kwa maana ya kuwakumbuka mashujaa wetu ambao walijitolea kwa roho zao katika kuleta ukombozi wa nchi yetu ni jambo la msingi sana.

Kuhusu bendera kupepea nusu mlingoti. Suala la bendera limewekewa utaratibu katika sheria ya kuwaenzi viongozi, nadhani inatosha na hakuna ulazima sasa kuingizwa katika sheria hii. Sote tunajua kwenye sheria ile ya kuwaenzi viongozi imeeleza vizuri utaratibu ule wa bendera kupepea nusu mlingoti, naamini inakidhi haja sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu tuipitishe sheria yetu hii ili tuwe na sheria iliyo bora zaidi inayosimamia vielelezo vyetu vinavyohusu bendera, nembo na wimbo wetu wa taifa.

Baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri tayari ametoa hoja sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wale wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, natumia Kanuni ya 63. Hivi sasa tumepokea karatasi nyengine nataka kuuliza tunaipitia ipi, ile ya mwanzo? Maana yake tusije tukachanganya madawa, tulizungumza mapema kama kuna marekebisho ya mswada urudi kwenye kamati ukajipange tena. Sasa nataka kujua muongozo wa kiti chako tuna miwili hivi sasa tunakamata huu tuliopewa hivi sasa au tuliokuwanao siku mbili tatu nyuma?

Mhe. Mwenyekiti, Sawa Mheshimiwa nimekuelewa, ni kwamba tunapitia wa mwanzo pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Kwanza

Masharti ya Awali

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar

Kifungu 3 Bendera ya Zanzibar pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4 Nembo ya Serikali pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 Wimbo wa Taifa wa Zanzibar pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6 Matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar pamoja na marekebisho yake
Kifungu 7

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, narudia tena uliza ujinga upate werevu, nataka nifahamu. Mhe. Waziri katufahamisha vizuri na kajitahidi kwa kiasi chake, hiki kifungu cha 7 nilikizungumza jana watu waachiwe kutumia nembo hii kutangaza Zanzibar. Hata Mhe. Mwenyekiti wangu makini Mhe. Ali

Suleiman Ali alizungumza kuna timu za mipira zinatoka, hata juzi timu ya Bunge tulikwenda Kenya tukapewa *tracksuit* na bendera zina nembo ya Tanzania. Suala hili tulikuwa tunalipigia kelele, kajitahidi Mhe. Waziri kueleza lakini vile vile ziada sio mbaya. Timu zetu za mipira kutangaza kuvaa fulana zikiwa na nembo za bendera ni kosa?

Vile vile maji umeyatia Bendera ya Zanzibar nayo ni makosa? Je, ndio tutakuwa tunautangaza utalii hivi? Nafikiri kilio changu kimeeleweka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwenye bendera tushapita sasa tuko kwenye nembo, kuitia nembo ya serikali kwenye alama yoyote ya biashara ni kosa, hatuwezi kudharau nembo yetu kwa sababu nembo yetu ina hadhi kubwa sana lazima tujue haitumiki kibiashara. Nembo yetu imesema kama kutakuwa na jambo la dharura muhimu ndio pale tunampa uwezo waziri wa kutumia kwa maslahi maalum yatakayotumika kwa ajili ya jambo maalum. Nafikiri haiwezi kutumika kibiashara ni jambo kubwa hili la nchi yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri lakini bado nafikiri hatujafahamiana au Kiswahili ninachokizungumza ni kizito. Nasema kama Timu ya Taifa ya Zanzibar inataka kuondoka sasa hivi kwenda nje ina alama ya bendera nayo ni makosa vile vile?

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub huko tumeshapita umesimama wakati sio, hicho kifungu tumeshakipita cha bendera sasa hivi tunazungumzia nembo. Hoja yake iko kwenye namba 7 si ndio? Hoja yako haipo kwenye kifungu namba 7.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kiangalie kifungu namba 7 chini kina vitoto a, b c, na d kimezaa hicho.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Mhe. Waziri alisema na jambo moja ambalo jana wajumbe wengi walilishauri wakati walipokuwa wakichangia hoja hii ni kwamba, Sehemu ya Pili ya ule mswada uliokuwepo ilikuwa imechanganya mambo yote matatu na hivyo ilikuwa haileti ufahamu mzuri pale Waheshimiwa Wajumbe walipokuwa wakiusoma ule mswada.

Ushauri uliotoka ni kwamba turudi ili sasa kila eneo tukaliwekee sehemu yake na hicho ndicho ambacho kimefanywa kwenye jadweli la marekebisho. Sasa hivi Sehemu ya Pili ndio ilikuwa inazungumzia Bendera ya Zanzibar na

matumizi yake ambayo tumeshapita. Sasa tunazungumzia Sehemu ya Tatu kwenye Nembo ya Serikali. Mhe. Jaku Hashim nadhani hoja yake ilikuwa aijenge kwenye Sehemu ya Pili ya mswada na hata akisoma ataona kuna marekebisho yamefanywa kwamba kuna maeneo waziri amepewa fursa ya kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kwa hivyo, sasa hivi nadhani tuko kwenye Sehemu ya Tatu ambayo inazungumzia Nembo ya Serikali na kwenye nembo sidhani kama anataka ifanyiwe biashara. Nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru pamoja na Mwanasheria Mkuu, ndio nilisema uliza ujinga upate werevu, lakini haya mambo yanatuchanganya, asubuhi tumepewa kitu chengine, jioni kitu chengine, unajua elimu zetu sisi ni ndogo. Mheshimiwa tuendelee.

Utaratibu

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, hata na mimi sijafahamu kwa sababu tumeambiwa tupo kifungu cha 7 kwenye mswada tuliopewa, ukiacha haya marekebisho tuliyopewa dakika 20 zilizopita. Sasa kwa heshima nauliza nifuate upi? Kwa sababu katika nambari 7 ya mswada tuliopewa *original* na mimi nina *concern* zangu ukiacha marekebisho tuliopewa dakika. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelekezo yako.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tunatumia mswada ule ule *original,* lakini ukitaka marekebisho kuna marekebisho katika jadweli ambalo tumepewa leo jipya, huo ndio utaratibu tunaoufuata.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sasa kama tunafuata jadweli hiyo basi itakuwa tuko *right* bado nambari 7 Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa tumeshakuelewa, Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sisi tunaheshimu sana mawazo wa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na jana walieleza vizuri sana na sisi tukakubaliana, walisema jana nakumbuka kabisa kifungu cha 7, walisema hapa tumechanganya kwamba ni marufukuru kwa mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa katika mambo yafuatayo. Sasa wao wenyewe wakashauri bendera iwe sehemu yake, nembo iwe sehemu yake na wimbo uwe sehemu yake. Sisi kwa kuwasikiliza wao na ndio maana tukaliomba Baraza lako kuakhirisha, lakini tungeweza kufanya majumuisho asubuhi ya leo kupata muda wa kuheshimu mawazo matukufu ya wajumbe ndio tukaja na jambo hili. Kwa hivyo,

Mheshimiwa sasa tumeshaingia Sehemu ya Tatu inayohusu nembo suala la bendera tumepita.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi tutakapokwenda kwenye timu yetu kwenye michezo kwa nchi nyengine wataondoka na bendera yetu ya Zanzibar na ndio maana tunampa uwezo Waziri kuondoa baadhi ya masharti, hayo ndiyo mambo yanayofanyika kwa maslahi ya nchi yetu na Taifa letu. Asante sana.

TAARIFA

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya (63) na (37). Mhe. Mwenyekiti, sote tunajenga nyumba moja mimi naamini kwamba bado tupo Kifungu cha 7, kwa vile sote tunajenga nyumba moja serikali na Wajumbe. Na huu Mswada umekuja dakika 20 zilizopita wa marekebisho, ningeomba kwa heshima kubwa ya kiti chako na sisi tutoe *concern* zetu kuhusu bendera yetu ya taifa. Mhe. Mwenyekiti, naomba ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa sasa hivi muda wa michango umepita, sasa tunapitisha vifungu, ukisema turudi kwenye michango ina maana mimi nirudi juu kule kwenye kiti changu ndio utaratibu ulivyo. Sasa hivi ni vifungu Mheshimiwa jana mlipata nafasi ya kuchangia na mkaleta marekebisho, mkasema marekebisho na Mhe. Waziri na AG, wameyafanyia kazi. Sasa tupitishe tu vifungu ndio kilichobakia hapa.

Kifungu cha 7

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, katika marekebisho tuliyopewa, kifungu cha 7 kina kitoto (a) - (h) kama sikosei kitoto (a) kinasema katika marekebisho;

"7. Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutumia Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar katika mambo yafuatayo:

a) kama alama ya biashara kwa ajili ya kitu chochote kinachouzwa au kinachotolewa kwa ajili ya kuuza,

b) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote kuuza, kuzalisha, inayouzwa au inayotolewa kwa ajili ya mauzo,

c) kuambatanisha juu ya bidhaa yoyote ya kuuza au kuzalisha, kwa mtu kufanya hivyo kinyume na madhumuni yanayozalishwa na Waziri..."

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshimiwa kwa vile sote tunajenga nyumba moja kwa hapa ningeomba kwa vile nchi za wenzetu tunaona kwamba bendera inatumika sio kama trade mark ya watu wangine lakini imo katika nembo za biashara. Tungeomba Mhe. Mwenyekiti kwa heshima yako serikali ikubali mtu atumie kwa idhini ya Waziri aweze kuitumia.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu (f) kama mapambo au mambo ya sanaa. Hili nchi za wenzetu limekuwa likiruhusiwa, kikombe unakikuta kimechorwa bendera ya Taifa ya nchi yao na wanaruhusu. Tunaona siku hizi wamasai wanafanya vitu vya bendera ya nchi yao wanaruhusu. Tumeona nchi yetu ya kitalii, huitangaza nchi yetu kupitia bendera ni jambo la busara na hiyo ndiyo sanaa. Ningeiomba serikali kwa hili iruhusu kama tulivyosema, Baraza lako la Tisa ni baraza ambalo sote ni Wanamapinduzi, tuna nia moja ya kujenga Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa jenga hoja yako, umalize ujibiwe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hoja yangu ni kwamba serikali iondoshe hii katika sanaa kifungu (f) kiondoke na huku kifungu cha (a), (b) na (c), iwe kwa ruhusa ya Waziri kunako masuala ya biashara. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kuna mengine ambayo unayoyazungumza tayari yameshafanyiwa marekebisho. Lakini kuna mengine ni mapya, sasa hayo mapya hatuwezi kuyafanyia kazi hapa wakati tunapitisha vifungu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu inabaki pale pale, namuheshimu sana ndugu yangu Mhe. Hassan Khamis. Kwa kuwa masuala ya Bendara ambayo wanayoyarudia tumeshapita, sasa hivi tupo kwenye Nembo. Mimi haya anayoyasema naomba awe mstahamilivu tuendelee. Kwa vyovyote itakavyokuwa kama kutatokezea umuhimu wa kuja kufanya marekebisho ya sheria huko mbele tukiona jambo hili linakwaza mambo yetu, tunaweza kuja kuyafanya hapa hayo yanayostahiki. Lakini kwa sasa jambo hili la mapambo na sanaa halileti sura ya hadhi na heshima kwa maana ya Bendera. Lakini nasema kwa sasa tupo kwenye Nembo, twende kwa mujibu wa taratibu humu ndani. Vyenginevyo itakuwa sisi wenyewe ndio tunaovunja utaratibu wetu. Ahsante sana.

Kifungu cha 7 Matumizi ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar kinyume na sheria pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 8

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitoa mawazo na serikali inaweza kuyachukua, kuyakubali au kuyakataa, Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora, madhubuti masharti ya sheria hii. Mawazo yangu yalikuwa kama hivi:

Vyama vya siasa vinapofanya mikutano wanaweza kuwa na bendera ya Zanzibar na wakaweka bendera yoyote ili kuleta umoja. Temeshuhudia juzi Marekani katika Kanuni mawazo yangu ana haki ya kuyachukua au kuyakataa, wala sishindani nae, ni ushauri tu. Kwa ajili ya kuleta ummoja wa nchi sijui nimefahamika. Kama patakuwa na bendera nyengine nyengine hapa na baendera ya Zanzibar iwepo ndio *priority*. Nafikiri nimefahamika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hapa ya bendera tumeshayamaliza, sasa ukinirudisha huko napata tabu kidogo. Kwa sababu sisi tumejiwekea utaratibu na kanuni kama hatujauheshimu tunapata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri amezungumzia nembo ndio anachokisema.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Amesema bendera.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Nembo au Bendera hebu rudia hoja yako?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Katika Kifungu cha 8 Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora au madhumuni ya sharti hili ndicho nilichokisimamia mimi. Nikasema nina mapendekezo anaweza kuyakubali au anaweza kuyakataa wala hakuna cha kushindana hapa ndicho hicho nilichosema mimi, katika kutunga kanuni.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jaku Hashim alisema hilo na akatoa mawazo yake lakini kwa vile Mhe. Waziri katika majumuisho yake hakuyataja hayo kama ameyatambua. Maana yake mchango wake wa kifungu hicho marekebisho hakukubaliana nayo, ndio utaratibu ulivyo. Kwa hivyo yeye ametoa maoni yake amesema alivyotaka lakini Mhe. Waziri katika

majumuisho akaona hakuna haja kwamba unapokwenda kwenye mikutano ya vyama vya siasa kutumia bendera ambayo matumizi yake yameelezwa vizuri kwenye sheria.

Nadhani hiyo ndiyo hoja ya Mhe. Jaku ambayo anayosimamia hoja yake, kwamba jana alishauri hivyo na nadhani Mhe. Waziri kwenye majumuisho yake ameona hilo halikuwa na haja ndio maana hakulitolea maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa ilikuwa Mhe. Waziri alitolee maelezo lisingekuwa ni hoja ambayo sasa hivi inaingiliwa tena. Mhe. Waziri labda ulitolee maelezo hilo la Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu amekwisha kuyamaliza kama ningekubaliana nayo ningeliyasema, ina maana sikubaliani nalo hilo. Kwa hivyo sikubaliani nalo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Asante sana Mhe. Mwenyekiti, kuomba kuna hiyari kukubali au kutokubali wala siwezi kulazimisha lakini haoni vile vile kama tunaivunjia hadhi au hatuipi nguvu bendera, maana ukiweka bendera hii pale moja inakuwa *constant* inakuwa kote kote ipo ikaja bendera hii ya Zanzibar ipo, ikaja hii ya Zanzibar ipo. Haoni kama jambo la kulifikiri.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tuendelee.

Kifungu cha 8 Uwezo wa Waziri wa Kutunga Kanuni pamoja na Marekebisho Yake

KIfungu cha 9

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa salamu zake nzuri. Hapa hatuoni kuwa Waziri tunampa nguvu kubwa na Mahakama zimeundwa na Katiba ya Zanzibar vile vile kuna mihimili mitatu haoni kama tunaingilia uwezo wa Mahakama.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa kama nilivyosema sisi ni wasikivu sana, ukisoma kifungu cha 18 tumefanya marekebisho kama ambavyo Mhe. Mjumbe anaeleza. Naamini ataona mazuri, makini kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu kifungu cha 18.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa kitu cha kupewa haraka haraka kina matatizo yake, lakini bado anielimishe 18 "Waziri anaweza kuondoa au kupunguza masharti chini ya kifungu cha 5, 8,10 na 12 cha Sheria hii kwa kuzingatia makubaliano na masharti kwa kadri atakavyoona inafaa", kiswahili hicho kadri atakavyoona inafaa anaweza akaona yeye inafaa, kumbe mwenziwe akaona haifai. "Kwa maandishi kwa mtu yeyote au kikundi cha watu kwa kikundi cha aina vitu vyovyote kwa masharti marufuku aliyoyataja kwa sheria"

Mimi ningeomba hapa hata Katiba hii ya Zanzibar inayoeleza mihimili mitatu hayaingiliani, tungeiwachia Mahakama ikaamua inavyotaka, leo polisi keshamkamata mtu kuhusu suala la kuvunja sheria atampeleka kwa Waziri moja kwa moja au atampeleka Mahakamani. Kajitahidi kapunguza kidogo lakini bado pana kitu kama kimejificha hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza Mhe. Jaku na nimemfahamu hoja yake ambayo anaijenga, lakini kama angesoma vizuri Mhe. Waziri hata kwenye sheria hii marekebisho ambayo yameletwa hakupewa mamlaka ya kufuta kosa au la kuondoa adhabu ambayo imewekwa na sheria hii. Hayo ni mambo ambayo yanafanywa na chombo kingine ambapo Mswada huu pamoja na marekebisho yake bado yametambua hayo. Uwezo ambao amepewa Waziri ni kwa yale maeneo ambayo ile sheria imempa mamlaka nayo kama yeye. Pia sheria imempa uwezo kwa mamlaka ile ile ya kupunguza yale ambayo yapo au kuzidisha yale ambayo yapo, ndiyo kifungu hichi kinavyosema kama haizungumzii adhabu wala hakizungumzii faini ambayo imewekwa. Hayo ni masharti yaliyowekwa na Mahakama kuamua.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 5, 8,10,12 ni uwezo aliyopewa Waziri na sheria ambao uwezo ule ule anapewa na kifungu hichi akona inafaa kupunguza yale masharti ya ule ukali ndiyo dhamira yake ya kifungu hiki wala haiyondoi masharti yaliyowekwa kwa upende wa Mahakama kutimiza wajibu wao wa kutoa adhabu au kutoza faini kwa mujibu wa sheria hii. Asante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, hapa pembeni ya Nam. 5 uwezo wa Waziri kuondoa au kupunguza masharti, kwa nini tusengeiwachia Mahakama moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti: Masharti yenyewe si ndiyo hayo ambayo yameandikwa humu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe Mwenyekiti, na mimi pia nina *concern* hapa hapa. Katiba yetu ya Zanzibar bado inaruhusu Serikali ya Umoja wa

Kitaifa na nikasema Baraza hili la Tisa tulilonalo ni Baraza la Wanamapinduzi watupu hamna Hizbu, lakini hatuwezi kujua 2020 itakuwaje, inaweza ikarudi Serikali ya Mseto tukapata Baraza lina Hizbu ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa hichi kipengele kumpa Waziri kuondoa na kila kitu mimi nafikiri sio kitu sahihi kwa sababu anaweza akaikosea bendera mtu wao ambaye anaendana na itikadi zake ikabidi amsamehe na huku keshai *abuse* bendera yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema uwezo huu tusimpe Waziri bora tuiwachie Mahakama ambayo inaweza kufanya kitu hichi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe tayari maelezo yameshaelezwa, Mwanasheria Mkuu ameeleza vizuri sana ni kwa yale ambayo Mhe. Waziri amepewa dhamana tu ndiyo ambayo anaweza kupunguza au kufuta vitu ambavyo amepewa mamlaka ya kufanya hivyo lakini sio vitu vyengine. Mnazungumzia vitu ambavyo sasa hivi naona kama hamjaelewa vizuri huu Mswada Mheshimiwa.

Kifungu cha 9 Waziri anaweza kusamehe kwa masharti au bila ya masharti pamoja na marekebisho Yake.

Sehemu ya Tatu

Makosa na Adhabu

Kifungu cha 10

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kifungu hichi wakati kwa upande huu kuna 13,14,15 na 16 mpaka 17 lakini katika gazeti letu la huku ni nambari 10. Nilimuuliza Waziri nataka anifahamishe kidogo alitoa maelekezo pale kwa mtu yeyote. Nilikuwa sijaifahamu hii kule tulipokuwa Mahakamani kuna kitu kinasema mimi mtu mzima mwenye akili timamu mwenye kitu gani. Sasa hapa nilichangia juzi kuwambia je, kuna watu wengine hutumia watoto katika kufanya vituko hivi hili tumeliwekaje, sikulisikia maudhui yake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Suleiman kwa maelezo yake, lakini mtoto, mtu mzima, mzee na kadhalika utaratibu wa sheria upo, anaevunja sheria atakwenda kwa mujibu wa kosa alilolifanya. Watoto wanawekewa utaratibu wao, watu wazima

wanawekewa utaratibu wao na kila mmoja hakuna aliyejuu ya sheria sote tupo kwenye utaratibu wa sheria.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sawa Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu cha 10	Kuikashifu Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu cha 11	Makosa ya Jumla Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu cha 12	Kufuta na Kubakisha Pamoja na Marekebisho Yake

(*Baraza linarudia)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ametoa hoja, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Bendera ya Zanzibar,
Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa
Zanzibar ya Mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afiri ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya mwaka wa 2016 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaulize wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa wanaokubali wameshinda. (*Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri kwanza nikupongeze sana kwa kupitishwa Mswada huu lakini vile vile niwapongeze na watendaji wako kwa kazi nzito ambayo wameifanya na niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao mbali mbali waliyoitoa katika kuhuisha na kufanya Mswada huu uwe bora zaidi kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Waheshimiwa Wajumbe mpaka kufikia hapa leo tumemaliza shughuli yetu, nitamuomba Mhe. Waziri, mnanipa ruhusa? Sasa niseme tu kwamba naakhirisha kikao chetu hadi Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:58 jioni Baraza liliahirishwa hadi Jumatatu tarehe 20/2/2017 saa 3:00 asubuhi)